# THE EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA

# MPANGO MKAKATI WA MIAKA 15

***"HABARI NJEMA KWA WOTE"***

**JANUARI 2020-DESEMBA 2034**

**Toleo la pili**

**YALIYOMO** **UKURASA**

MAELEZO YA VIFUPI .................................................. 5
1. MCHAKATO WA KUANDAA DIRA .................................................. 12
2. UMUHIMU WA MIPANGO NDANI YA EAGT .................................................. 14
3. NGUZO NA VIPAUMBELE .................................................. 16
3.1 NGUZO TATU ZA VIPAUMBELE .................................................. 16
3.2 VIPAUMBELE SABA .................................................. 17
4. MAONO, DHIMA NA MAADILI .................................................. 18
4.1 MAONO YETU .................................................. 18
4.2 DHIMA YETU .................................................. 18
4.3 MAADILI YETU SABA YA MSINGI .................................................. 18
5. MIKAKATI YETU 12 YA KITAIFA .................................................. 20
6. MALENGO YETU 12 YA MUDA MREFU .................................................. 22
6.1 KUHUBIRI INJILI .................................................. 22
6.2 KUIMARISHA UONGOZI .................................................. 26
6.3 ELIMU YA TEOLOJIA .................................................. 28
6.4 HUDUMA ZA JAMII .................................................. 29
6.4.1 Huduma za Jamii nje ya Kanisa .................................................. 29
6.4.2 Huduma za Jamii ndani ya Kanisa .................................................. 30
6.5 KUJENGA MAOFISI .................................................. 33
6.6 KUMILIKI ARDHI .................................................. 34
6.7 KUMILIKI MAWASILIANO .................................................. 35
7. MPANGO WA FEDHA .................................................. 37
7.1 KUJENGA HAZINA .................................................. 37
7.2 MATUMIZI YA HAZINA YA TAIFA .................................................. 39

7.3 UTARATIBU WA MAKUSANYO YA SADAKA ........................ 40
8. MPANGO WA UTEKELEZAJI ................................................ 41
8.1 KIPINDI CHA MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI ..................... 41
8.2 KALENDA YA MIAKA 15 ...................................................... 42
8.3 MAJUKUMU YA KURUGENZI ............................................... 44
8.3.1 Shughuli za kurugenzi ................................................... 44
8.3.2 Muhtasari wa majukumu na mwelekeo ............................ 45
8.4 MAJUKUMU YA KANDA ....................................................... 45
8.5 MUUNDO WA UTEKELEZAJI MMK-15 .................................. 46
8.5.1 Umuhimu wa muundo unaoendana na MMK-15-KMP .... 46
8.5.2 Kanisa la Mahali Pamoja ................................................ 46
8.5.3 Mgawano wa majukumu kwa vipaumbele- Jimbo ........... 47
8.5.4 Mchoro wa muundo ngazi ya Taifa ................................. 49
8.5.5 Majukumu ya Sekretariati ............................................... 49
8.5.6 Wajumbe wa Sekretariati ................................................. 50
9. MPANGO WA UFUATILIAJI .................................................. 50
9.1 TAKWIMU MUHIMU ........................................................... 50
9.2 MATOKEO YA MMK-15 ....................................................... 52
9.2.1 Matokeo ya miaka 15 ..................................................... 52
9.2.2 Maelezo ya Matokeo ....................................................... 53
9.3 TAARIFA ZA MIEZI MINNE NA MWAKA ............................... 54
9.3.1 Viashiria-vigezo Muhimu kwa Jimbo ............................... 54
9.3.2 Kutoa taarifa na kupanga kila mwaka ............................ 55
9.4 VIGEZO ILI KUFANIKISHA MMK-15 NA MIPANGO ............... 55
10. WASHIRIKI KATIKA MCHAKATO WA KUANDAA MMK ........... 58

**ORODHA YA MAJEDWALI** **UKURASA**

Jedwali 1 Washiriki na tarehe za Warsha ........................................... 12
Jedwali 2 Vipaumbele vya ngazi zote ................................................ 17
Jedwali 3 Kalenda ya Kipindi cha Maandalizi....................................... 42
Jedwali 4 Kalenda ya vipaumbele miaka 15......................................... 43
Jedwali 5 Muhtasari wa majukumu ya Kurugenzi................................ 45
Jedwali 6 Viashiria vya fuatilia utendaji ............................................... 54
Jedwali 7 Vigezo vya lazima ili MMK-15 na Mipango ifanikiwe............. 56

## MAELEZO YA VIFUPI

| | |
|---|---|
| CGM | Christ Gospel Messenger |
| CWI | Chipukizi wa Injili |
| Dkt. | Daktari |
| EAGT | The Evangelistic Assemblies of God Tanzania |
| ESBC | Eastern Southern (Zonal)Bible College |
| KIA | Kilimanjaro International Airport |
| KEM | Kurugenzi ya Elimu na Mipango |
| KMP | Kanisa la mahali Pamoja |
| KUSK | Kurugenzi ya Uimbaji sifa na Kuabudu |
| Mch. | Mchungaji |
| MF 3 | Mpango wa Fedha wa miaka 3 |
| MK-2 | Mipango Kazi ya miaka miwili |
| MMK-15 | Mpango Mkakati wa miaka 15 |
| MMS | Mipango na miradi inayoendelea sasa. |
| MUT-3 | Mpango w a ufuatiliaji wa miaka mitatu |
| Mwl. | Mwalimu |
| MYM | Mipango ya Majimbo |
| PAE | Pan Africa Evangelism |
| Rev. | Reverend |
| TAG | Tanzania Assemblies of God |
| TEBE | The Evangelistic Board of Evangelism |
| WHI | Wanaume wa Huduma ya Injili |
| WWI | Wanawake wa Injili |

## NENO LA MWALIKO KUTOKA KWA ASKOFU MKUU

***Ninakusalimu kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo!***



Kwa kipindi kirefu sasa Kanisa la "The Evangelistic Assemblies of God Tanzania" (EAGT) limefanya kazi kubwa ya kueneza Injili ndani na Nje ya nchi ya Tanzania toka liliposajiliwa rasmi tarehe 18, Julai 1991. Hatua kwa hatua Mungu mwenyewe ameliongeza Kanisa, mwaka hata mwaka na hadi sasa lina washirika wengi walio ndani ya Makanisa na matawi yake zaidi ya 4000 yaliyoenea nchi nzima kwenye Majimbo 81 na Kanda 9 hadi Juni 2019.

Ninamrudishia Mungu utukufu, heshima na shukrani kwa kujiletea mavuno hayo. Tangu EAGT ilipoanza huduma nchini; chini ya Uongozi wa hayati Mch. Dkt. Moses Samuel Kulola, uongozi wa Kanisa umeendelea kujengeka toka Taifa hadi Kanisa la Mahali Pamoja (KMP) kwa mfumo wa kuanzia Askofu Mkuu, Maaskofu wa Kanda, Maaskofu wa Majimbo na wachungaji wa Kanisa la Mahali pamoja na ofisi zao. EAGT katika kuboresha utendaji wake husimamia Neno la Mungu na inayo Katiba yenye Imani ya dhehebu na Misingi ya Imani. Kanisa pia limekutana na changamoto mbalimbali lakini kwa msaada wa Mungu (Ayubu 2:10) zimetufundisha mengi, na Bwana ametuvusha!

Kuanzia mwezi wa Oktoba 2018 hadi Juni 2019, Kanisa la EAGT limepitia mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka 15 (MMK-15) ijayo kwa ajili ya sasa na vizazi vinavyofuata. Mpango utakuwa na vipindi 4; kipindi cha maandalizi, kikifuatiwa na vipindi vitatu vya miaka mitano mitano kuanzia Januari 2020 hadi Desemba 2034.

EAGT ina Imani moja ya Mungu Mmoja nafsi tatu; Biblia moja; Katiba moja na sasa dira moja! Kwa hiyo Dira (MMK-15) yetu sasa ni moja na maono yetu ni; "Habari njema ya wokovu imewafikia watu wote nchini Tanzania na Nje ya Nchi" (Warumi 1:16-17). Tuna Maadili ya

msingi saba yanayogusia; ibada; zaka na sadaka; sifa na kuabudu; kufunga na kuomba; Neno la Mungu; kuwaleta watu kwa Yesu na shukrani kwa Mungu. Tuna nguzo tatu nazo ni; Utakatifu, Uongozi; na Utoaji zikibeba Vipaumbele saba vinavyohusiana na; kuhubiri Injili; kuimarisha Uongozi; elimu ya Teolojia; Huduma za Jamii, kumiliki Ardhi; Ujenzi wa Ofisi za utawala na kumiliki Mawasiliano. Tuna mikakati 12 ya kitaifa na Malengo 12 yatakayofikiwa kutokana na shughuli mbalimbali.

Kwa ajili ya kujenga mshikamano na nguvu ya umoja wetu tutajenga Hazina ya Taifa kwa kufungua na kuendesha “Akaunti ya Maendeleo‟ kutokana na sadaka za viongozi, washirika na rafiki zetu. Tumejiwekea matokeo makubwa 7 ikiwemo; kanisa letu kukua mara nne likihubiri Injili iliyo hai, wachungaji wetu kuwa na elimu ya teolojia kutoka Vyuo vyetu au nje, watoto wetu kusoma sekondari, kujenga shule za seminari, awali na msingi, makanisa yetu kuwa na majengo ya kudumu na ofisi na kumiliki vyombo vya vyetu vya habari na vitega uchumi.

Ninakukaribisha usome, ufahamu na utekeleze Mpango Mkakati wa EAGT wa miaka 15. Pamoja na huu soma pia Mpango Kazi wa majimbo na Kanda wa miaka 2 ya kwanza. Tukisema kwa kauli moja; *“Kanisa langu, EAGT yetu, Habari Njema kwa wote”*. Kama Paulo alivyoandika; neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu. Yote hayo yafanyike katika Upendo (Waebrania 10:24).

Mtumishi mwenzako katika Ofisi ya Yesu Kristo.

Rev. Dkt. Brown Mwakipesile,
Askofu Mkuu wa Kanisa la EAGT,
Dodoma-Makao Makuu ya EAGT- Juni 2019

## NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA KATIBU MKUU



Nakusalimu kwa Jina la Bwana Yesu Kristo. Ninamshukuru Mungu kwa kuliwezesha Kanisa la EAGT kuweka vipaumbele saba katika kuandaa Mpango Mkakati wa miaka 15 (Dira), mipango ya Majimbo na Kanda ikiwemo na mipango mingine ndani ya Kanisa kupitia mchakato wa ushirikishwaji wenye hatua 15. Mchakato umehusisha viongozi, wachungaji na washirika wengi wa EAGT.

Awali ya yote napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati Kuu, Wajumbe wa Halmashauri Kuu, Wajumbe wa Baraza la Waangalizi, Wadhamini wetu, Wakurugenzi wote wa Idara na Ofisi zao ngazi ya taifa katika Kanisa letu na Wakuu wa Vyuo vyote vya EAGT ambao wameshiriki katika kuandaa dira hii. Wote ninawashukuru sana na Mungu awabariki sana!

Washiriki wa majimbo waliweza kukusanya maoni na kuweka Mipango ya Majimbo wakishirikisha Wachungaji, viongozi wengine na washirika wao, kwao nasema Mungu awabariki. Nawashukuru pia wahudumu wote, hasa wa Kanisa la EAGT Mlimwa West-Dodoma na Mchungaji wao, wazee wa Kanisa waliohakikisha warsha na semina za maandalizi zinafanikiwa; kama vyombo vya sauti, usafi, umeme, upishi, na madreva wote wa watumishi wa Mungu, Bwana ninayemtumikia awaongeze na awaongezee.

Mwisho lakini si kwa umuhimu ninamshukuru sana Mwl. Dkt. Binagwa Fulgence kwa juhudi zake za kuandaa na kuendesha warsha na semina zote za maandalizi na kuandika dira kwa kutumia maoni ya washiriki chini ya Uongozi wa Askofu wetu Mkuu. Kwake yeye na familia yake aliyotumia muda wao karibu miezi minane; nasema Mungu awabariki.

Kama Mtendaji Mkuu wa Kanisa la EAGT, ninatarajia tutajitoa kikamilifu, (Warumi 12:1) tutaenenda sawasawa na mipango yetu tuliyoiandaa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu kuanzia sasa, huku tukiwa na swali kuu ndani ya mioyo yetu kama Mitume wa Bwana Yesu Kristo walilokuwa nalo; “Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?” (Yohana 6: 28) Ni maombi yangu sasa kuwa; Mungu Baba Mwenyezi atusaidie kutenda kile ambacho tumekitaabikia kwa muda mrefu ili hatimaye tutimize maono yetu; “Habari njema ya wokovu iwafikie watu wote nchini Tanzania na nje ya nchi”.

Kwa kauli moja tuseme; “*Kanisa Langu, EAGT yetu, Habari njema kwa wote”.*



Askofu Dkt. L. M Mwizarubi
Katibu Mkuu wa Kanisa la EAGT
Dodoma-Makao Makuu ya EAGT- Juni 2019

# NENO KUTOKA KWA MWEKA HAZINA MKUU



Ninakusalimu kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo! Kuanzia sasa hadi Miaka 15 ijayo, Kanisa la EAGT limejiwekea vipaumbele na malengo ya muda mrefu ndani ya Mpango Mkakati ngazi ya Taifa na Mipango ya muda mfupi katika ngazi za Kanda, Jimbo na Kanisa la Mahali Pamoja. Ni ukweli usiopingika kuwa ili kufanikisha vipaumbele vya Kanisa letu na kuyafikia malengo Kanisa linahitaji raslimali za aina mbalimbali hasa raslimali watu na fedha (Mhubiri 10:19).

Kwa hiyo moja ya hatua muhimu ya Kanisa ni "kujenga Hazina ya Taifa" au kuimarisha uwezo wa kifedha wa pamoja kwa ajili ya kufanikisha na kuyafikia malengo ya Kanisa kwa wakati uliopangwa; pia ni njia ya kujenga mshikamano wetu hasa kupitia sadaka. Kwa vile Mungu aliisha sema "fedha ni mali yake na dhahabu ni mali yake" (Hagai 2:8), kila mshirika anao wajibu wa kujitoa na kutoa kiasi alichojaliwa, kama kutimiza moja ya nguzo zetu za dira hii, yaani „utoaji". Kufuatana na jinsi ambavyo "uongozi" utakuwa ukifanya maamuzi na kutoa mwelekeo kila inapohitajika.

Jambo kubwa katika Utoaji ni uaminifu na usimamizi wa dhati kutoka ndani ya dhamira safi. Kanisa tumefanya mengi lakini kwa umoja wetu tutafanya makubwa zaidi, kwa sababu kwa Mungu hakuna lisilowezekana. Sasa ni wakati wa kuwa na nidhamu binafsi katika kutekeleza hayo tuliyokubaliana ili kuijenga hazina ya Kanisa letu kwa kuendesha "Akaunti ya Maendeleo" chini ya Uongozi wa Askofu Mkuu. Wakati huo tukiimarisha mifumo ya makadirio, makusanyo, matumizi na taarifa zetu, tukitumia raslimali fedha kwa uangalifu na uaminifu, chini ya waweka hazina, wahasibu na wakusanya sadaka wetu.

Ninawashukuru kwa kutenda kama mtakavyokusudia mioyoni mwenu, na fanyeni kwa moyo (Wakolosai 3:23-24) ili tufikie maono yetu; “Habari njema ya wokovu imewafikia watu wote nchini Tanzania na Nje ya Nchi”.

Kwa kauli moja tuseme; “*Kanisa Langu, EAGT yetu, habari njema kwa wote”.*

Mungu Awabariki



Rev. Dkt. PrayGod Mgonja
Mweka Hazina Mkuu-Kanisa la EAGT
Dodoma-Makao Makuu ya EAGT- Juni 2019

## 1. MCHAKATO WA KUANDAA DIRA

Mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka 15 (Dira) ulianza Tarehe 10 Mwezi wa Oktoba 2018, pale Dodoma baada ya EAGT kuanzisha Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo ili kuendeleza dhehebu la EAGT. Vikao vya awali vilifanyika kama sehemu ya hatua 15 ambazo zingefuatwa mpaka MMK-15 kuzinduliwa rasmi tarehe 27 Juni, 2019 Alhamisi, Makao Makuu ya EAGT Dodoma. Askofu Mkuu kwa kushirikiana na Kamati Kuu walipitisha wazo la awali na mchakato wa hatua zote. Maaskofu wa Kanda zote na Makatibu wa Kanda kwa mwaliko wa Askofu Mkuu tarehe 4 Januari 2019 waliidhinisha mchakato huo kwa niaba ya Halmashauri za Kanda.

Mwaliko maalum kutoka kwa Askofu Mkuu ulipelekwa kwa mkono wa Katibu Mkuu kwenda kwa Wadhamini, Maaskofu na makatibu wote wa majimbo 81, Makamu Askofu na waweka Hazina wa Kanda zote, Wakurugenzi wakuu, Makatibu na waweka hazina wa kurugenzi zote. Pia Wakuu wa vyuo walialikwa kuhudhuria warsha ya kujenga uwezo.
Kwa sababu ya nia (Wafilipi 2:2-4) ya kuwa na mpango shirikishi, washiriki waligawanyika katika makundi manne yenye wajumbe kutoka Kanda zote 9 na Majimbo 81, kama ifuatavyo;

**Jedwali 1 Washiriki na tarehe za Warsha**

| | KANDA/KURUGENZI | TAREHE ZA DIRA YA TAIFA | TAREHE ZA MIPANGO YA MAJIMBO |
|---|---|---|---|
| I. | Nyanda za Juu kusini Kati<br>Nyanda za juu kusini Mashariki<br>Ziwa Rukwa | 5 na 6 Machi 2019 | 30April, 1-2Mei 2019 |
| | Kurugenzi ya KUSK | | |
| | Chuo cha Mbeya na Mdhamini | | |
| II. | Kanda ya Kaskazini<br>Kanda ya Kati | 8 na 9 Machi 2019 | 14-16 Mei 2019 |
| | Kurugenzi ya CGM | | |
| | Chuo cha Kongwa/Dodoma/KIA | | |
| III. | Kanda ya Ziwa Magharibi<br>Kanda ya Ziwa Mashariki | 19 na 20 Machi | 14-16 Mei 2019 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kanda ya Magharibi | 2019 | |
| | Kurugenzi za WWI/CWI | | |
| | Chuo cha Biharamulo/Tarime/Tabora | | |
| IV. | Kanda ya Mashariki Kusini | 22na 23 Machi 2019 | 7-9 Mei 2019 |
| | Kurugenzi za WHI, TEBE, Elimu na Mafunzo | | |
| | Chuo-ESBC-Morogoro-Mdhamini | | |
| V. | Viongozi wa Kurugenzi zote ngazi ya Taifa na Wakuu wa Vyuo | Kama hapo juu | 17 na 18 Mei |
| VI. | Mrejesho wa Rasimu MMK-15 kwa Halmashauri Kuu | | 30-31 Mei na 1 Juni 2019 |
| VII | Kuzinduliwa kwa Mpango Mkakati-15 na Mipango Kazi ya Jimbo, Kanda na KMP | | 27 Juni 2019 |

**Warsha ya kujenga uwezo:** Warsha hiyo ilifanyika kama tarehe hapo juu ili kuwapa wajumbe fursa ya kuchambua mazingira, kujadili maadili, kuweka maono na dhima, kuweka vipaumbele, mikakati na malengo na shughuli za kitaifa. Pia na kujiandaa kukusanya maoni na kuandaa mipango ya Majimbo.

**Kukusanya maoni:** Wajumbe wote kutoka majimboni walipata fursa ya kukusanya maoni na kukusanya takwimu kutoka kwa Wachungaji na wengine, ili kuandaa rasimu za mipango ya Majimbo.

**Warsha ya Pili ilifanyika kama tarehe zinavyoonesha hapo juu.** Kusudi ilikuwa ni kujadili Mipango ya Majimbo pamoja na MMK-15, na kuhakikisha vipaumbele vya Kitaifa na Jimbo havipingani. Pia mjadala ulikuwa na majadiliano ya Mipango ya Kanda.

**Warsha ya Kurugenzi na Vyuo:** Warsha ya siku mbili tarehe 17-18 Mei iliandaliwa kwa ajili ya kujadili wajibu wa kurugenzi na Vyuo katika utekelezaji wa MMK-15 na Mipango ya Jimbo.

**Mrejesho kwa Halmashauri**: Baada ya rasimu za MMK 15 na mipango ya majimbo kuandaliwa; Halmashauri Kuu chini ya Askofu Mkuu iliketi kwa siku mbili Mei 30 na 31, 2019, ili kupokea, kujadili na kutafakari rasimu ya MMK-15 (Dira) na Mipango ya Majimbo. Msistizo ukiwa ni wajibu wa uongozi; Kamati kuu na Kamati Halmashauri za Kanda katika utekelezaji wa MMK-15 na Mipango mingine.

**Washiriki:** Siyo rahisi kuandika orodha ya washiriki wote lakini itoshe kuweka orodha ya majina ya washiriki katika mchakato ngazi ya Taifa - angalia sura ya 12. Na kama kwa bahati mbaya Jina halikuonekana itakuwa ni kosa la kibinadamu.

## 2. UMUHIMU WA MIPANGO NDANI YA EAGT

Kuna umuhimu wa EAGT kuwa na Mipango kwa sababu zifuatazo:

a. Mchakato wa kuandaa na kutekeleza Mipango huleta umoja na mshikamano (Matendo ya Mitume 2:42) ndani ya EAGT, kwa sababu washirika na viongozi hunia mamoja, (Wafilipi 2:2) na hushiriki katika kuendeleza EAGT. (Amosi 3:3 na Zaburi 133:1)

b. Mpango Mkakati wa miaka 15 (MMK-15) na mipango kwa ujumla huwa ni fursa ya kuelekeza imani, (Waebrania 10:38, 11:6, Waefeso 6:16 ), na maombi (Mathayo 18:19-20, Waefeso 6:18) ya EAGT, na tunapojibiwa huwa ni rahisi kutambua majibu (Marko 11:24-25) na hivyo kumshukuru Mungu na kumrudishia utukufu (Zaburi 29:1-2).

c. Mipango ni kiungo cha mawasiliano kati ya washirika wa EAGT na uongozi, kati ya KMP na jingine, kati ya Jimbo na Jimbo na kati ya Kanda na Kanda. EAGT na EAGT ya nje ya Tanzania, kati ya EAGT na serikali na taasisi nyingine za kiroho na kijamii. Hivyo hurahisishia wengine kufahamu maono (Habakuki 2:2), malengo, shughuli na nafasi ya EAGT katika Taifa.

d. Mipango kwa ujumla wake, huunganisha nguvu na vipaji vilivyomo (1Wakorintho 12:12, Waefeso 4:11-12) ndani ya EAGT na

vipaumbele vya EAGT ili kutumia raslimali zote za Kanisa (mawazo, muda na kipato), kwa ajili ya kutoa huduma kwa Washirika, Wahitaji na majirani wa karibu na wambali (Mathayo 25:40).

e. Mipango hutafsiri na kutekeleza Katiba ya EAGT, au ni kiunganishi cha viongozi wa sasa na wajao pamoja na wadhamini, na washirika katika utekelezaji wa kazi tuliyoitiwa (Mathayo 18:19-20), itasaidia EAGT kutenda yale tuwazayo, na tusemayo (Zaburi 19:14) katika vitendo (Yakobo 1:22, 4:17, Mathayo 5:16).

f. Mipango ya ufuatiliaji wa miaka 3 (MUT-3) itasaidia kufuatilia, kupima, kutathmini na kupeana mrejesho (Luka 10:17-19, Yakobo 3:17, Waefeso 4:29, Yohana 17:12, 22) kuhusu utendaji (Mathayo 25:19) ufanisi, changamoto na maendeleo ya Kanisa kwa ujumla wake. Hii hutoa fursa ya kujifunza na kutumia uzoefu ili kupanga na kusonga mbele.

g. Mipango (MMK-15) ni fursa ya kuandaa malengo ya muda mrefu, (Isaya 46:10) ili kwa mfano kama kuna miradi ya muda mrefu: hati fungani (miaka 7-10), ujenzi, viwanja vikubwa na mashamba, miti, mazao ya biashara kama korosho, ununuzi wa viwanja, ujenzi wa vyuo, muda huo unatosha kusimamia na kuonamatunda yake (faida-riba) itakayopatikana ndani ya kipindi hicho. (Mt 25:20-21)

h. Malengo ya MMK-15 kuhusu watoto (Kumbukumbu la Torati 6: 6- 10, Kumb. 4:6), (Mithali 22:6) na vijana, yanatoa maandalizi ya watoto (Mithali 20:7, Mithali 23:13-14) na vijana (1 Timotheo 4:13) kuishi maisha bora kwa kuliishi neno la Mungu. Na Jinsi Mungu apendavyo (2 Timotheo 3:15).

i. Mipango ya utekelezaji (MU-3), inatafsiri malengo ya muda mrefu ya kitaifa (MMK-15), katika malengo ya muda wa miaka mitatu - Kanda/Kurugenzi, na Mipango kazi ya Jimbo (MK-2), inaandaa malengo ya muda mfupi na shughuli za kuyafikia, mwaka 1 KMP. (Luka 14:28-32)

j. MMK-15 utakuwa na awamu nyingi, ikiwemo kuanzisha na kutekeleza mchakato wa kuboresha na kutunisha mfuko wa maendeleo, kujenga tabia ya kuweka akiba na mtaji, ili kujenga na

kuimarisha nguvu ya umoja wetu EAGT (Zaburi 133:1, Waefeso 4:4-6), kuwa na mifumo ya uwazi, uwajibikaji wa pamoja (Mathayo 19:19) na mrejesho wakati muafaka kwa ajili ya maendeleo makubwa na kuanzisha shule za awali katika KMP.

k. Mpango wa ufuatiliaji na tathmini (MUT-3) unatumia viashiria, malengo na takwimu zilizopo (Hesabu 1:2), kupima ufanisi wetu na kufanya marekebisho au masahihisho katika malengo ya muda mrefu na mfupi ya MMK-15, MU-3, MK-3.

l. Mipango ya Kanisa la Mahali Pamoja (KMP) (Matendo ya Mitume 2:42, 47, 20:7), ndiyo nguzo yakuchangia kukua kwa washirika, kuwaimarisha katika utakatifu na utoaji wakiimarishwa na Mipango ya Jimbo, yenye kutilia mkazo utekelezaji na usimamizi kwa usimamizi wa Mipango ya Kanda ya Uongozi.

## 3. NGUZO NA VIPAUMBELE VYA MPANGO MKAKATI

### 3.1 NGUZO TATU ZA VIPAUMBELE

Kutokana na semina elekezi mambo matatu yamejitokeza ambayo ni nguzo za mipango ya EAGT.

I. **UTAKATIFU:** (1 Petro 1:15-17, Waebrania 7:26; 12:14, 2 Timotheo 2:21, Waefeso 1:4-5, Tito 2:3: 1 Wathesalonike 3:13, 2:10, 4:4-5; Zaburi 16:3).

II. **UONGOZI:** (Kolosai 3:16-17, 22; Kutoka 18:19, 21-22; Yohana 12:26, 1 Petro 5:1-4, Kumbukumbu 1:15- 17). Tito 3:1-2; Waebrania 13:17).

III. **UTOAJI**: (2 Wakorintho 9:6-12, 2Wakorintho 8:1-4, Luka 6:38) Waebrania 13:16, 11:4; Warumi 12:1)

## 3.2 VIPAUMBELE SABA

Kutokana na historia ya EAGT na uchambuzi wa mazingira, mawazo na maoni ya washiriki, pamoja na hali halisi ya EAGT, vipaumbele vifuatavyo vimejitokeza kama jibu la matokeo ya tafakari hiyo.

**Jedwali 2 Vipaumbele vya ngazi zote**

| | KIPAUMBELE | TAIFA | KANDA | JIMBO | KMP |
|---|---|---|---|---|---|
| I | KUHUBIRI INJILI -(Kuhubiri Injili iliyo hai na yenye nguvu)- Kanisa zima | | V | V | V |
| II | KUIMARISHA UONGOZI (Kuwajenga viongozi watende sawa na ngazi zao)-Kanda | | V | | |
| III | ELIMU YA TEOLOJIA (Kuimarisha Chuo Kikuu cha Biblia/na Vyuo vya Kanda) | V | | | |
| IV | HUDUMA ZA JAMII (Kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo, ndani nan je Kanisa)-Kanisa zima | | | V | V |
| V | KUJENGA MAOFISI(Kujenga makao makuu na kumbi, maofisi ya Kanda na Majimbo-Kanisa zima | V | | | |
| VI | KUMILIKI ARDHI (Kumiliki maeneo ya ardhi kwa ajili ya huduma za Jamii na ujenzi wa Makanisa)Viongozi | V | V | V | V |
| VII | KUMILIKI MAWASILIANO (Kumiliki Vyombo vya habari) -Kanisa zima | V | | | |

Kwa vile ni vigumu kutekeleza vipaumbele bila raslimali, chini ya mpango wa fedha, EAGT itashughulika na KUJENGA HAZINA yaani kutunisha Mfuko wa Maendeleo kupitia kufungua na kuendesha Akaunti ya Maendeleo, na Kanisa zima litahusika chini ya Uongozi wa Askofu Mkuu.

# 4. MAONO, DHIMA NA MAADILI

## 4.1 MAONO YETU

Habari njema ya wokovu imewafikia watu wote nchini Tanzania na Nje ya Nchi (Warumi 1:16, Isaya 55:11; Luke 4:18-19, Habakuki 2:2-3)

## 4.2 DHIMA YETU

Dhima ya kufikia maono ni; EAGT tutakuwa Kanisa moja (Waefeso 4:4-7) lenye nguvu za kiroho za kutenda, kumiliki na kuwafikia maelfu ya watu kwa Neno la Mungu, tukiwafundisha kuyashika yote aliyosema Yesu Kristo ili kuwa na Jamii imara iliyofanikiwa kiroho, kiafya, kifikra (Joshua 1:8, Zaburi 119:15, Wafillipi 4:8, Malaki 3:16), kiuchumi, na mambo yote (3Yohana 3) na hatimaye wateule wapate Uzima wa Milele; (Wakolosai 1:28; Yohana 12:26; Luka 4:21-22; 1Wakorintho 4:1-2)

## 4.3 MAADILI YETU SABA YA MSINGI

(2Timotheo 2:15, 1Wakorintho 14:40)

### Imani ya EAGT

Imani ya dhehebu la EAGT iko ndani ya Katiba yake na ni sehemu ya Misingi ya Imani. Dhehebu la EAGT linaamini Mungu mmoja katika nafsi tatu ambaye ni BABA wa wote wamchao aliyeumba Mbingu na Nchi. YESU KRISTO Kristo mwana wa Mungu ni njia pekee ya wokovu kwa wanadamu wote. Ubatizo wa ROHO MTAKATIFU ni ahadi ya waliopokea wokovu huo.

### Misingi ya Imani ya EAGT

- Katiba ya EAGT imeainisha Misingi ya Imani yake, ambayo hufundishwa kwenye Vyuo vyake vya Teolojia (rejea Katiba ya EAGT). Kuifuata Misingi hiyo ni sehemu mojawapo ya Maadili ya Msingi.
- Kanisa linawajibu wa kuilinda, kuifundisha, kuitetea na kuifuata.
- Chuo nje ya EAGT kinachofundisha elimu ya teolojia tofauti na misingi hiyo hakitatambuliwa na EAGT.
- Mafundisho kinyume na hiyo Misingi ya Imani itajumuishwa kama imani potofu na haitakubalika katika Kanisa la EAGT.

- Mchungaji wa Kanisa la Mahali Pamoja anao wajibu wakuisimamia na kuifundisha kila inapowezekana.

**Umuhimu wa Maadili ya msingi**

- Maadili ya msingi yanalenga kujenga tabia na mwenendo maalum wa washirika wa EAGT nchi nzima.
- Yanarahisisha na kutofautisha yaliyo sahihi katika mwenendo wa mshirika siku hadi siku.
- Yazingatiwe ili kuonesha EAGT iko kwenye mwelekeo sahihi
- Watoto wazoezwe kuyakariri na kufanya kwa kujifunza kutoka kwa wazazi wao.
- Mshirika anapoyatimiza hayo, ndani yake anaonesha uaminifu, utiifu, uwajibikaji, kujali na kuwa tayari.
- Mchungaji ahakikishe kila mshirika anayafahamu na hatua ya kwanza ni kuyakariri yeye na washirika.

**Maadili ya Msingi 7**

Yamechaguliwa Maadili ya msingi SABA, kwa kuzingatia namba saba ni ya ukamilifu. Wanandoa, wajane, vijana, wanawake na wanaume, wanaweza kuongeza maadili juu ya haya: TAHADHARI endapo yataongezwa yasifanane, yasipingane na hayo, ila yawe nyongeza na yasisimame kama mbadala wa haya 7, inashauriwa yasiongezwe.

**Kila mshirika atayasoma hivi:**

***Mimi Mshirika wa Kanisa la EAG (T) ninahaidi kwamba:- (Kumbukumbu la Torati 23:23)***

**IBADA**

i. Nitahudhuria Ibada zote zilizopangwa, muda uliopangwa na kwa utaratibu wa EAGT. (Waebrania 12:14, Waebrania 10:25, - Zab 122:1, Mdo 1:14)

**ZAKA NA SADAKA**

ii. Nitamtolea Mungu zaka na sadaka kufuatana na maandiko (Malaki 3:10-11, Mithali 3:9-10).

**SIFA NA KUABUDU**

iii. Nitamsifu na kumwabudu Mungu katika Roho na Kweli (Zaburi 100:1-3, Yohana 4:23, Zaburi 150:2-3)

**NENO**

iv. Nitasoma, nitalitafakari, nitaliishi Neno la Mungu (Waebrania 4:12; Joshua 1:8, Zaburi 119:97) na maisha ya utakatifu (1Petro 1:15- 16), Warumi 15:4; 2Timotheo 3:16).

**KUFUNGA NA KUOMBA**

v. Nitafunga na kuomba kwa imani kufuatana na neno la Mungu (Mathayo 17:21, Esta 4:15-16)

**KUSHUHUDIA**

vi. Nitawaleta watu kwa Yesu na kuwafanya wanafunzi wake sawa na Agizo kuu(Mathayo 28:19-20, Mt 9:37, 1 Timotheo 1:15, Ezekieli 3:17-18

**SHUKURANI**

vii. Nitamrudishia Mungu sifa, heshima, utukufu na shukrani kwa ajili ya wema wake (1Wathesalonike 5 18; Zaburi 50:23; Ufunuo 4:11)

## 5. MIKAKATI YETU 12 YA KITAIFA

i. <u>Kuwaleta watu kwa Yesu</u> kupitia njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya Injili (Marko 16:20), kushuhudia, umishemi na maisha ya utauwa (Mathayo 5:16) yatabaki ndilo kusudi la EAGT kuwepo, yaani kulitekeleza Agizo Kuu la Yesu Kristo (Mathayo 28:19) na kuwafundisha Neno la Mungu (Mathayo 28:20), Kwa Msaada wa Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 1:8, na kutumia Jina la Yesu (Mdo 2:21, Mdo 3:6).

ii. Kuimarisha <u>mshikamano</u> na umoja wa EAGT bila kukiuka Katiba; Kanisa la Mahali Pamoja lijitambue pia kama sehemu ya EAGT Taifa, badala ya kuendeshwa kama huduma binafsi (Ministry) (Matendo ya Mitume 2:46-47, Waefeso 4:3-5), likijua nguvu yetu iko katika umoja wetu.

iii. Kuongeza ushirikishwaji wa kila muumini katika kujenga na kuimarisha hazina ya Taifa ili kufanikisha vipaumbele vya Kitaifa (Mdo 2:44-45, 2Wakorintho 9:7)

iv. Kila mchungaji aijue dira ya EAGT, ayakariri maono, ayafundishe na kuyasimamia maadili 7 ya msingi (2Timotheo 2:2, 1Timotheo 4:11) awe chachu ya mabadiliko.

v. Uongozi wa Jimbo uvijue vipaumbele vya kitaifa na nafasi ya Jimbo katika kuvitekeleza, akiwa pamoja na uongozi wajue Jimbo lao linaelekea wapi, katika kutekeleza malengo na shughuli za Jimbo.(Tito 1:5, 2:1)

vi. Mchungaji asiridhike kuona baadhi ya washirika wake hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu na kutojiendeleza kielimu. Na ikiwa elimu yake Mchungaji ni ya Msingi, alazimike kuchukua hatua madhubuti ya kujiendeleza hadi Kidato cha Nne kwa masomo ya muda mfupi (QT-Mtihani wa Maarifa). (Mithali 4:13, Ufu wa Yohana 1:3)

vii. Wachungaji wote wa EAGT wasio na elimu ya teolojia, wachukue hatua za makusudi kwenda vyuo vya teolojia, ili kuongeza ufahamu wao wa Elimu ya Ki-Mungu (Mithali 9:9, Mithali 2:6, 12:1, Mithali 2:2)

viii. EAGT ipambane na umaskini kwa kuwekea mkazo washirika kupenda kufanya kazi, na kuhakikisha kila muumini ana shughuli halali ya kumwingizia Kipato. (Mithali 20:4, Hagai 2:8, Zaburi 113:7, Kumbukumbu 28:12, Mithali 31:17-18,Muhubiri 3:22, Warumi 4:4, Waefeso 4:28). Mtu haokoki maskini kuendelea kuwa maskini kanisani.

ix. Mbinu zitaendelea kufanywa ili kuwaibua, kuwaombea na kuwaonesha njia washirika wenye vipaji, ujuzi, taaluma, na uwezo wa kiuchumi, ili washiriki kikamilifu katika kufikia malengo ya Kanisa (1 Wakorintho 12:12-14, waefeso 1:7, 4:11-12, 1 Wafalme 5:15-17). Kila mtu ni sehemu ya mwili wa Kristo.

x. Juhudi za makusudi zitafanyika kubadili mtazamo na msimamo wa kushindwa, woga na kutothubutu ili kuwa na mawazo chanya ya maendeleo ya kiroho na kimwili. (Wafilipi 4:13, Luke 1:37, 2 Wakorintho 10:5, Zaburi 19:14, 2 Timotheo 1:7)

xi. Askofu wa Jimbo na ofisi yake wanaowajibu wa kuitambulisha EAGT katika ngazi husika ya Serikali na kujenga mahusiano bora. Kuzifahamu sera za nchi, fursa zilizopo, kuwatii na kuwaombea viongozi ngazi husika kwa faida ya Washirika wa EAGT. (Tito 3:1- 2, 1 Timotheo 2:1, Warumi 13:1-7, 1 Petro 2:13-15 na 7)

xii. Kanisa linao wajibu wa kutoa huduma za Jamii, popote lilipo na kila kiongozi atambue kuwa jinsi miaka inavyosogea ardhi inakuwa adimu, jitahada zaidi ziwekwe kuimiliki ardhi kwa ajili ya majengo ya Kanisa ya kudumu, miradi ya maendeleo ya ustawi wa jamii. (Mathayo 25:34-40, Yakobo 1:27, 2:26)

## 6. MALENGO YETU 12 YA MUDA MREFU

### 6.1 KUHUBIRI INJILI

**Utangulizi**

Kusudi maalum la EAGT kuanzishwa ni kulitekeleza Agizo kuu la Bwana wetu Yesu Kristo (Mathayo 28:19-20; Marko 16:20) kwa maana Mungu hapendi mtu hata mmoja apotee (1 Timotheo 1:15, Luka 19:10; Ezekieli 3:17-18 & 33:8). Jambo hili ni kwa Msaada wa Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 1:8, Warumi 8:26-27). Yesu Kristo anataka watu waisikie Habari Njema (Warumi 10:17; Mathayo 24:14) na kuwa Wanafunzi wa Yesu. Waujali wokovu (Waebraina 2:3) na kuishi maisha ya Utakatifu (1 Petro 1:15). EAGT kwa msaada wa Roho Mtakatifu imepeleka habari njema sehemu nyingi za Nchi na Nje ya nchi lakini bado inatakiwa Injili iliyo hai iendelee kuhubiriwa kwa nguvu na nguvu za Mungu (Matendo ya Mitume 8:7-8, 8:39) zidhihirike katika maisha ya waaminio (Matendo ya Mitume 5:15). Kwa sababu hii, Katiba ya EAGT (IBARA YA IV kifungu cha 2 Toleo la 2011) imeweka wazi nafasi ya KMP kuhubiri Injili; "kutii na Kuhubiri Injili kamili ya YESU KRISTO".

Uchambuzi wa mazingira umeonesha uwezo wa EAGT wa kuhubiri Injili ni uwepo wa mtandao mkubwa wa makanisa machanga na ya zamani karibu ya 4000 yaliyoenea nchi nzima. Huu uwezo utatumika kwa kila mshirika kushuhudia na kuwaleta watu kwa Yesu na kanisa kuongezeka (Mdo 5:14,). Kila mshirikia mmoja au wawili kuleta mtu mmoja kwa Yesu kila mwaka. Itapimwa kwa upande wa vijana wa Huduma ya Injili (VWI). Tanzania kuna amani na utulivu ambayo ni fursa nzuri ya kupeleka Injili kwa Jina la Yesu (1 Timotheo 2:1) na hata kama washirika watapata ugumu, wao wafurahi tu (Mdo 5:41). Ni fursa ya kuwaleta watu kwa Yesu na maovu yapungue, nchi iwe na amani na utulivu zaidi.

Fursa nyingine ni miundombinu inayoeendelea kuboreka ya barabara, reli na mawasiliano ya kimtandao, hii inarahisisha kupeleka Injili sehemu zote Tanzania. Kuhubiri Injili iliyo hai kutapambana na imani potofu, mmomonyoko wa maadili, mambo ambayo yamejitokeza katika uchambuzi wa mazingira. Imani za kishirikina, uchawi na kuabudu mizimu, ibada za sanamu na nguvu za giza zitapambanishwa na Jina la Yesu nazo zitashindwa. Kwa hiyo:-

**Lengo la 1**

**Kuihubiri Injili iliyo hai ya kuwafanya watu wawe wanafunzi wa Yesu ili Kanisa liongezeke na watu waokolewe. (Marko 16:20; Matendo ya Mitume 26:16-18)**

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Kuwaibua washirika wenye wito wa kuwa Wainjilisti makanisani na kuwajengea uwezo waliopo tayari (Waefeso 4:11)
ii. Kuanzisha kozi za muda mfupi wa wiki moja hadi tatu katika Vyuo vya Biblia ili kufundisha au kuwakumbusha somo la Injili na Uinjilisti kwa Wainjilisti.
iii. Kila Kanda kuwa na vyombo vya Injili ambavyo vinaweza kutumika majimboni na hata makanisa ya Mahali pamoja kila inapohitajika.
iv. Kuwakumbusha na kuwaelekeza washirika umuhimu wa ushuhudiaji (Kwa mfano kutumia Maandiko mfano: Warumi 6:23, 1Yohana 1:9, Isaya 1:18, Luka 15:7, Warumi 10:9, Yohana 3:18, Yohana 14:6, Waebrani 4:12 nk)

v. Kuwa na utaratibu wa kuwafuatilia waliokoka katika mikutano ya Injili unaoonekana kudhoofika katika baadhi ya maeneo ndani ya saa 48 (Mdo 20:20-21)
vi. Kila baada ya kipindi maalum taarifa ya kazi ya Injili ipelekwe Jimboni kutoka Kanisa la Mahali pamoja
vii. KMP kuandaa mikutano ya Injili angalao mara moja kwa mwaka kwa kutumia Wainjisti wa KMP au Jimbo.
viii. Kuwatambua wachungaji au wainjilisti wenye mzigo wa utume ili kuwawezesha watumike zaidi.
ix. Kila Jimbo kusaidia au kufungua matawi mapya 2 kila mwaka au zaidi kufuatana na malengo yao.
x. Injili ya Nyumba kwa nyumba iwekewe kipaumbele na ibada za nyumbani au maeneo pali inapostahili.

**Lengo la 2**
**Kuwafanya waliompokea Yesu kuwa wanafunzi wa Yesu na kuwafundisha kushika yote (Mathayo 28:20, Wakolosai 3:16).**

**Utangulizi**
Kanisa la EAGT limejiwekea utaratibu mzuri wa kuhakikisha washirika wanapata mafundisho ya Neno la Mungu (Joshua 1:8) wakitumia Biblia yenye vitabu 66, hii ni kufuatana na Katiba (IBARA YA IV kifungu cha 3 Toleo la 2011). Kila siku ya Jumatano KMP huwa na Ibada ya kujifunza Biblia. Jumapili asubuhi muda wa saa moja hutengwa kwa ajili ya Shule ya Jumapili kwa kutumia vitabu maalum.

Kila ibada kuna sehemu ya Neno la Mungu, yote haya yakilenga kuwaimarisha washirika katika kulijua Neno la Mungu (1Timotheo 3:16). Kuwaandaa kwa ajili ya kulisoma, kulitafakari na kuliishi Neno la Mungu kama moja ya Maadili saba ya Msingi (Zaburi 119:105) katika Dira hii. Pamoja na hayo kuna wakristo wapya wanaingia kanisani na kuokoka. Lakini pia uchambuzi umeonesha dalili kuwa bado kuna kiu ya neno la Mungu. Kwa mfano kuhamahama kwa washirika kutoka Kanisa hili kwenda jingine, kuhudhuria mikutano ya madhehebu mengine inaweza kuwa ni kiashiria kuwa kuna upungufu katika mafundisho wayapokeayo (Tito 2:1). Lakini pia inawezekana mafundisho ni manyonge hasa kufuata mkumbo wa Injili ya Mafanikio na Miujiza (Yohana 20:31).

Uchambuzi wa mazingira umeonesha pia kuna athari za utandawazi, imani na mafundisho potofu (1Timotheo 1:3-4) kama vitisho vya imani yetu. Jingine ni washirika kuwa watalii wa kanisa moja hadi jingine, na mlipuko na wingi wa madhehebu ambavyo huleta ushindani usio na tija na wakati mwingine hata mgawanyiko. Haya yote yatashughulikiwa na mafundisho sahihi kuanzia KMP, semina za Idara, na vyuo vya teolojia. Neno kutoka Waefeso 2:20-23, Yohana 1:3, Mathayo 7:25, 16:18), linaweka dhana nzima ya msingi kama Kristo na Mitume kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Kila KMP liweke mkazo wa mafundisho ya Neno la Mungu kwa madarasa ya waongofu wapya kuwalea na kuwabatiza mapema. (1Wathesalonike 2:13)
ii. Shule za Jumapili za watoto (CWI) zipewe kipaumbele. (Kumbukumbu la Torati 6:7-9)
iii. Wachungaji wafanye juhudi kuwaibua na kulea vipawa vya Ualimu/Uinjilisti makanisani
iv. Vyuo vya EAGT viwe na kozi fupi kuanzia wiki moja hata zaidi kuwakumbusha walimu mbinu za kufundisha, wakati kozi maalum (cheti -astashahada au stashahada ya walimu inaandaliwa)
v. Sehemu ya matoleo ya Shule ya Jumapili itengwe kwa ajili ya Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo, ambayo itasaidia pia matumizi ya kawaida ya Vyuo vya Biblia
vi. KMP lihakikishe Jumatano inatumika vema kujifunza Biblia ikiwemo Misingi ya Imani ya EAGT na Maadili 7 ya Msingi.
vii. Mafundisho maalum yawe yanatolewa kuhusu athari za utandawazi hasa kwa vijana na watoto (1Wakorintho 3:3, Waefeso 5:8, 11-12, 15-16, Warumi 1:22)

## 6.2 KUIMARISHA UONGOZI

### Utangulizi

EAGT inaongozwa na Neno la Mungu (Kumb 31:7, 23, Joshua 1:6-9) kwa maana ya "Imani ya Dhehebu" na Misingi ya Imani inatokana na Maaandiko (Biblia). Na katika shughuli zake za kila siku EAGT itafuata Maono na Maadili 7 ya Msingi yanayotokana na Maandiko (2Timotheo 3:16-17).

EAGT ina mfumo wa uongozi toka ngazi ya Taifa hadi Kanisa la Mahali Pamoja. Hizo ngazi hurahisisha mawasiliano, maamuzi na utendaji wake (Kutoka 18:20-22, Kumbukumbu la Torati 1:15). Kanisa linazo pia Kurugenzi (Idara) mbalimbali kama sehemu ya kuboresha utendaji, nazo huanzia ngazi ya Taifa hadi KMP. Mchungaji ndiye kiongozi wa KMP akisaidiwa na Wazee, Mashemasi na viongozi wa Idara kufuatana na Katiba. Mchungaji anawajibika kwa Halmashauri ya Jimbo chini ya Askofu wa Jimbo, ambaye pia huwajibika kwa Askofu wa Kanda na hatimaye kwa Askofu Mkuu. Askofu Mkuu ndiye Mchungaji wa Kanisa la EAGT chini ya Mchungaji Mkuu Yesu Kristo (1 Petro 5:4). Kila mtu hustahili kuchungwa. EAGT inao mfumo mzuri wa kufanya maamuzi kwa njia ya kuendesha vikao mbalimbali kufuatana na Katiba yake. Viongozi huwekwa kwa mujibu wa Katiba kwa kuchaguliwa au kuteuliwa pale inapobidi. Kila inapostahili semina elekezi hufanywa kwa viongozi wote wapya hata wa zamani.

Kutokana na uchambuzi wa mazingira (Sura ya 3) imedhihirika kuwa baadhi ya wachungaji huona KMP kama huduma binafsi (Ministry) au mali yao, japo kwa kiasi fulani Katiba imetaja hali hiyo. *(Ibara ya IV-MADHUMUNI kifungu cha 2' -Toleo la 2011)*. Uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya viongozi wana majukumu mengi au mgawanyo wa majukumu si sawia. Jambo ambalo hudhoofisha ufanisi wa utendaji na yaweza kuathiri afya ya mhusika na kutafsiriwa kama upendeleo kwa walio wachache.

Pamoja na manufaa ya kurugenzi (idara), imeonekana hazishirikiani katika kupanga na kutenda, miongozo haiwasiliani, kuna mwingiliano wa majukumu na uteuzi haukuzingatia uwezo wa baadhi ya viongozi. KMP linalalamika kwa kuelemewa na michango kutoka ngazi za juu. Mahudhurio ya wanachamana ni changamoto kubwa ya Idara.

Uchambuzi pia umeonesha hitaji kubwa la kuimarisha uongozi na utawala katika ngazi za kuanzia Kanda, Jimbo hadi KMP na Idara ngazi zote. Katika moja ya mapungufu yaliyojitokeza wazi ni kutotunza kumbukumbu yaani Kanisa kutowekea mkazo nafasi ya kutafuta na kutumia takwimu katika kupanga na kulinda urithi wa historia ya changamoto na mafanikio ya EAGT. Ni ushauri wa kitaalamu kuwa baada ya Mpango Mkakati ni muhimu sana Uongozi na Utawala uandaliwe upya ili kuendana na malengo ya Dira mpya ya EAGT, kusudi ya kukabiliana na changamoto mpya. Kwa hiyo;-

**Lengo la 3**

**Kujenga na kuimarisha uwezo wa viongozi ngazi zote kufanya maamuzi kwa kutumia takwimu na kwa msaada wa Roho Mtakatifu**.

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Kuchagua maeneo maalum na mahsusi ya uongozi na utawala yatakayoongeza maarifa ya Uongozi na utawala.
ii. Kuandaa viongozi wa Ngazi ya Kanda na au Jimbo ili nao wakafundishe viongozi ngazi ya Jimbo na KMP.
iii. Kumtaka kila mchungaji ahudhurie semina mbili au zaidi za uongozi kwa mwaka ili kumnoa katika uongozi na utawala.
iv. Kila mchungaji aandae mafundisho ya kuboresha uongozi wa Wazee wa Kanisa, mashemasi na wasaidizi wake wengine.
v. Kila Kanisa liwe na mpango wa miaka miwili kufuatana na vipaumbele vyao na vya Taifa.
vi. Vyuo viandae masomo ya siku 3 hadi wiki moja ya Uongozi kwa wachungaji na wakurugenzi, wazee na viongozi wa Idara
vii. Kuwahamasisha wachungaji kujiendeleza, hasa waliomaliza darasa la msingi kusoma ili wafikie kidato cha nne (QT).
viii. Kuboresha utendaji wa kurugenzi kwa kushirikiana baina yao, katika kupanga, kuandaa miongozo ya Idara mbalimbali kufuatana

na Mpango Kazi na kuendesha semina, warsha na makongamano sawa na Mpango Kazi wa Jimbo na Kanda

ix. Kurugenzi zishirikiane katika kuweka mkazo wa maendeleo ya wanawake, wanaume, vijana na watoto na wachungaji wao.

Kila Mchungaji na kila kiongozi, kila wakati ajiulize; „je mimi ni mfano kwa ninao waongoza? (Mathayo 5:16) Katika utoaji, utakatifu, maadili, kutunza muda, kujua maono, vipaumbele vya taifa, na matokeo ya kitaifa?

## 6.3 ELIMU YA TEOLOJIA

### Utangulizi

Kwa kipindi kirefu sasa EAGT imejitahidi kuboresha elimu ya teolojia kwa watumishi wake kwa kuanzisha na kuendesha Vyuo vya Teolojia vya Kanda na Taifa. Kuna vyuo vya Kanda; Chuo cha Kanda ya Mashariki Kusini (ESBC) kilichopo Morogoro, Chuo cha Kanda ya Magharibi kilichopo Tabora, Chuo cha Tarime cha Kanda ya Ziwa Mashariki na Chuo cha Biharamulo cha Kanda ya Ziwa Magharibi. Chuo cha Mbeya kwa ajili ya Nyanda za Juu. Chuo cha Kongwa cha Kanda ya Kati, na Chuo cha KIA cha Kanda za Kaskazini. Vyuo hivyo huendeshwa kwa ushirikiano na Majimbo ya Kanda nzima chini ya Uongozi wa Askofu wa Kanda, na shughuli za kiutawala huongozwa na Mkuu wa chuo. Kuna Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Teolojia ambacho sasa kinatoa ELimu ya shahada ya Teolojia kikiwa na makao makuu Jijini Dodoma.

### Lengo la 4

**Kuboresha elimu ya Teolojia ili kila Mchungaji awe na stashahada na Shahada ya kwanza ifikapo 2034.**

**Mikakati na shughuli** (Mithali 9:9; 23:12; 8:33)

**6.3.1** Uongozi wa juu kuelekeza Wachungaji ambao wamesimikwa na hawajaenda chuo cha Biblia wafanye hivyo.

**6.3.2** Kuboresha na kuimarisha Vyuo vya Kanda hatimaye viwe ni matawi ya Chuo Kikuu cha Teolojia cha Taifa.

**6.3.3** Kuunganisha Vyuo vya Kanda kiutendaji ili kuongeza wanafunzi, ubora na ufanisi.

**6.3.4** Kuimarisha Chuo Kikuu cha Teolojia cha Taifa ili kiandae walimu kwa ajili ya Vyuo vya Kanda.

**6.3.5** Vyuo vya Kanda vianzishe pia mafunzo ya Astashahada ya Teolojia.

**6.3.6** Vyuo vya Kanda vianze kutoa kozi fupi maalum kwa Wainjilisti, Waalimu wa Biblia wiki mbili hata kufikia nne.

**6.3.7** Vyuo pia viwe na michepuo ya kozi za waweka Hazina wa Majimbo na Uongozi, na wakusanya sadaka, na vifundishe lugha ya Kiingereza.

**6.3.8** Vyuo vya Kanda viwasiliane na Serikali kuendesha mitihani ya Maarifa (QT).

**6.3.9** Katika kipindi cha mpito EAGT iingie ubia au ushirikiano na vyuo vingine vyenye Imani kama yake kutoa elimu nyongeza au isiyo EAGT.

## 6.4 HUDUMA ZA JAMII

### 6.4.1 Huduma za Jamii nje ya Kanisa

Kama ilivyokwisha elezwa katika maeneo mengine ya vipaumbele na malengo, EAGT imeanza kutoa Huduma za Jamii (Zaburi 41:1-3, Wagalatia 2:10) nje na kuhubiri Injili ambayo kwayo ni sehemu muhimu sana ya Huduma za Jamii ikiwemo kuhubiri watu waache maovu na kuanzisha makanisa kwa ajili ya huduma za kiroho, ushauri wa kichungaji na ushauri nasaha. EAGT kufuatana na mikakati ambayo imeisha tajwa, inatambua umuhimu wa afya, maji, elimu, lishe bora kwa washirika na watanzania kwa ujumla wake. Hazina ya Taifa itatenga asilimia fulani kwa ajili ya huduma ya jamii. Uzoefu wa kuanzisha shule ya Sekondari unaonesha kuwa gharama nyingi ni za awali.

Uchambuzi wa mazingira umetambua mapungufu kuhusu eneo hili; ukianzia ndani ya Kanisa inaonesha kuwa Kanisa la EAGT lina uwezo mdogo wa kiuchumi, ujuzi na uzoefu wa kutoa huduma hizo, japo lina uwezo mkubwa wa wataalamu ambao hawajaibuliwa na kupata fursa ya kutumia ujuzi wao. Uchambuzi pia unaonesha kuwa Kanisa limezungukwa na makundi maalum yenye mahitaji mengi ya kimwili pia. Lakini pia hata wale wanaompokea Yesu, wengine wanaendelea kuwa sawa na makundi maalum, na hivyo kuhitaji huduma nyongeza na kuombewa. Changamoto nyingine ni kukosa utaratibu wa kuyatambua

makundi hayo pamoja na kuwa wataalamu wenye ujuzi huo wamo makanisani. Kanisa limewekea mkazo kutoa kuliko kutafuta na kufanya kazi.

**Lengo la 5**

**Kuanzisha miradi mbali mbali ya Huduma za Jamii ikiwemo; elimu, afya na maji**

**Shughuli Muhimu:** (Wafilipi 4:19; Mathayo 25:40; Zaburi 68:5; Mithali 19:17, Isaya 1:17)

i. Kila Kanisa la Mahali Pamoja lenye watoto zaidi ya 20, lianzishe Shule ya Awali kufuatana na taratibu za Serikali
ii. EAGT kuimarisha na kuipanua Shule ya Sekondari ya Kahama ili kuweza kusajili watoto wengi zaidi
iii. Kila Kanda kuanzisha shule ya Msingi moja ambayo baada ya miaka 7 itakuwa na Seminari
iv. Kila Kanisa lenye washirika zaidi ya 1000, lianzishe shule ya Msingi kufuatana na utaratibu wa Serikali lakini kwa nyongeza ya maono ya EAGT.
v. Kila Kanda (yaani majimbo yote) kuchimba kisima kimoja katika wilaya mojawapo kwa mwaka au kusaidia shule mojawapo ya Serikali.
vi. Baada ya kupata eneo la kutosha, KMP lenye washirika zaidi ya 2000 lianzishe zahanati au shule ya Sekondari
vii. Waalimu wote wa watoto wahitimu cheti cha ualimu wa watoto.

### 6.4.2 Huduma za Jamii ndani ya Kanisa

Pamoja na kuwa Kanisa linapenda kutoa Huduma za Jamii kwa makundi maalum na wananchi kwa ujumla nje ya Kanisa, lakini pia lenyewe linakabiliwa (Wagalatia 6:9-10, Waefeso 3:32) na uwezo mdogo wa kiuchumi na changamoto za elimu ya kutoa huduma hizo. Pamoja na nia nzuri ya Kanisa kupenda kusaidia, lakini pia linakabiliwa na changamoto ya uwezo mdogo wa elimu kwa upande wa baadhi ya watumishi na baadhi ya washirika. Hali ya washirika na watoto wao haina tofauti kubwa na wahitaji walio nje ya Kanisa pamoja na kuwa linamtumikia Mungu

(Marko 10:28-30). Hali yake kijamii iko nyuma kwa sehemu kubwa wakati mwingine mbaya zaidi kuliko nje ya Kanisa. Wakati watu walioitwa kwa jina lake ni warithi wa baraka za Ibrahimu (Wagalatia 3:14 na 3:29), na wanatii (Isaya 1:19). Mungu amehaidi kuwainua watu wake (Zaburi 113:7)

Dalili za lishe duni hasa kwa watoto chini ya miaka 5 zinaonekana ndani ya baadhi ya makanisa na wengine wana dalili za utapia mlo. Familia nyingine hushindwa kukidhi mahitaji ya milo miwili kwa siku ambazo si za kufunga na kuomba, na wamekuwa ni sehemu ya asilimia 49.1% ya watanzania maskini waishio chini ya dola 1.9 ya Marekani mwaka 2011. Kuna ufukara mkubwa wa kipato na mawazo, kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watu wazima na hata badhi ya vijana.

Uwezo mdogo wa kiuchumi, ujuzi na uzoefu wa washirika na Kanisa kwa ujumla wa kutoa huduma uko chini. Kuna mtazamo pia wa baadhi ya watumishi kufikiri haiwezekani mtu akawa na mahitaji muhimu halafu akampendeza Mungu. Uchambuzi wa mazingira umeonesha kuwa, uwezo mdogo wa kiuchumi wa washirika unahusiana na uwezo wa Kanisa, na hali hii ni kitisho kwa kanisa, na inatakiwa mikakati ya kujihami, na kwa hiyo washirika wanakuwa tegemezi kwa Kanisa kuwapa ufumbuzi wa matatizo yao, badala yao kuleta ufumbuzi wa matatizo. Baadhi ya washirika wamejikita kwenye kupokea miujiza wakati wote, kufutiwa madeni, na kusahau haki huja na wajibu wa kufanya kazi (2Wathesalonike 3:8, 10-12, 1Wathesalonike 4:11-12, Waefeso 4:8).

Kwa hiyo wengine huhama hama kuitafuta miujiza kwa kuambiwa wapande mbegu kila mahali waendapo (Yohana 20:30). Ni wazi pia kuwa kuna tatizo katika uwiano wa huduma na ongezeko la washirika. Kanisa letu linaongezeka kwa kasi na hasa watoto wanaongezeka na watu wanaokoka, hii imeleta changamoto ya upungufu wa maeneo ya kuabudia na vifaa vya huduma kanisani.

EAGT imeunda kurugenzi ya Chipukizi wa Injili (CWI) ikitarajia huduma ndani ya Kanisa kuwajenga watoto ambao muda si mrefu ndiyo Kanisa la kesho. Mafundisho yao huendelea kila Jumapili hii ni hatua njema. Kwa kuwashirikisha waumini matatizo na changamoto zinazowakabili wataweza kuboresha mawazo na mtazamo wao. EAGT sasa inahitaji watoto wenye afya njema na lishe bora, ili kuboresha uwezo wa kufikiri.

Vijana wengi hawajapata mwelekeo kimaisha, wanahitaji mwongozo na msaada wa kujitambua. Walio vyuoni hujikuta wanajiunga tu na makundi ya vijana wa madhehebu mengine wakati mwingine yenye kufundisha imani potofu .

**Lengo la 6**

**Kuboresha hali za maisha ya washirika Kanisani kupitia Huduma za Jamii**

**Mikakati na Shughuli za kufikia lengo**
(Wafilipi 2:3; Mdo 2:44-46; Mdo 4:34-36)

i. Kanisa la MP litambue familia zenye hali ngumu kwa kutumia Idara mbalimbali na kutafuta chanzo kwa kutumia takwimu za Kanisa.
ii. Kila KMP liwe na utaratibu wa kuboresha lishe ya watoto k.m kuwaandalia uji watoto wenye umri chini ya miaka 5 kila Jumapili.
iii. Washirika wajenge tabia ya kujiwekea akiba japo kidogo kila siku ili kujenga mtaji wa baadaye.
iv. KMP liunde SACCOS, VICOBA au vikundi vya kuchangiana na kuwajibishana.
v. Wachungaji na viongozi ngazi ya Jimbo ikibidi nao wawe sehemu ya mfano katika kuunda vikundi (2Wathesalonike 3:7-9) vyao.
vi. Watu wasiojua kusoma na kuandika na kuhesabu, watambuliwe na kuanzishiwa masomo (KKK).
vii. Kila mshirika ajulikane anaishi maisha gani na awe na shughuli halali yakumwingizia kipato.
viii. KMP lianzishe Shule ya Awali endapo watoto wako zaidi ya ishirini -45), kwa ajili ya malezi yao. (Neno, afya, utoaji, usafi, akiba heshima kwa wazazi na miili yao n.k).
ix. Pale inapowezekana Kanisa lianzishe mradi wa Kanisa kwa pamoja au kusaidia hasa vijana kuanza shughuli zao halali kuwaingizia kipato.
x. Kanisa liwatambue wajane, yatima, wazee na wale wenye uwezo mdogo ili kuwa na mpango wa kuwasaidia.
xi. Kila KMP lenye uwezo lichimbe kisima cha maji pale ambapo hakuna, au kusaidia kulipa gharama za kuvuta maji.

xii. Wachungaji wawe mstari wa mbele kuhamasisha na kuwa na Bima za Afya, wasio nazo.
xiii. Semina za ujasiriamli, uchumi, mahusiano-ndoa na ushauri nasaa kwa watoto wa wachungaji, mzazi mmoja, wajane nk zipewe kipaumbele na si hiari.
xiv. Wachungaji na washirika wenye utayari wajiunge kwenye kundi la kutunisha mfuko ile kuwa na mradi mkubwa wa kitega Uchumi ngazi ya Jimbo, Kanda au Taifa.

## 6.5 KUJENGA MAOFISI

Kufuatana na muundo na utendaji wa Kanisa la EAGT, kuanzisha Makao makuu ya EAGT kumekumbana na changamoto mbalimbali. Hii ni pamoja na Kanda, Majimbo na hata baadhi ya Makanisa ya Mahali pamoja hayakuwa na maofisi, au mahali salama pa kuweka kumbukumbu, kufanya mikutano na ofisi za utawala. Shughuli za kiofisi za Askofu Mkuu, Katibu Mkuu, Mweka Hazina Mkuu, Askofu wa Kanda na Askofu wa Jimbo vile vile kwa kiwango fulani zilihama kufuatana na wapi alipo kiongozi. Hii ni eneo ambalo uchambuzi wa mazingira umeanisha kama mapungufu, hasa kutokuwa na mfumo thabiti wa kutunza kumbukumbu. Eneo hili litawekwa chini ya lengo la kumbukumbu na ufuatiliaji. Jitahada za kuanzisha Makao makuu kwa kununua majengo Dar-es-salaam, zimeisha elezwa chini ya lengo jingine.

Ofisi yoyote lazima iwe na anwani kamili lakini pia kwa kuhusisha swali la kumiliki ardhi, ofisi zitahitaji kuwa na eneo la kutosha ambapo pia shughuli nyingine zinaweza kufanyika. Ikumbukwe pia mwanzo ofisi hailengi kuwa ni jengo kubwa, ofisi hutengenezwa na utaratibu mzima wa kuweka kumbukumbu na taarifa za watumishi na shughuli za Jimbo kanda na KMP na si majengo ya kifahari.

Kwa kulitambua hili, tayari EAGT imefanikiwa kumiliki eneo Jijini Dodoma - Mwangaza. Rasimu ya ramani zimechorwa na kufanya malipo ya uchoraji upande wa makao makuu. Kuna mpango wa kujenga Ukumbi ambao unaweza kuchangiwa na Wachungaji, waalimu, wamissionari, na wengine watakaopenda kuwekeza. Faida ikatumika katika kuwasaidia wachungaji, uwekezaji, bima za afya, moto, maendeleo nk (kama masomo yao au kwa watoto wao, kustaafu). Idara ya WWI inaendesha hosteli kama mradi wa Wanawake Tanzania, utaratibu huu unaweza

kufuatwa na ujenzi wa Ukumbi.

**Lengo la 7**

**Kuboresha mazingira ya utendaji na utawala wa Kanisa la EAGT**

**Shughuli muhimu za kufikia malengo**

i. Kuendeleza ujenzi wa Ofisi za makao makuu kutokana na Hazina ya Taifa (akaunti ya maendeleo).
ii. Kujenga Ukumbi wa Kanisa la EAGT Jijini Dodoma kutokana na Hazina ya Taifa.
iii. Kila Kanda kumiliki eneo na kiwanja halafu kujenga ofisi ya Kanda.
iv. Kujenga kumbi, hosteli, hoteli au na vitega uchumi vingine vya Kanda, Jimbo au KMP baada ya vile vya Kitaifa.
v. Kila Jimbo kujenga Ofisi za Jimbo ambayo itatunza kumbukumbu za kila Kanisa.
vi. Kila KMP kuwa na ofisi ambayo itatunza takwimu na taarifa za washirika
vii. Uongozi kuwapa semina fupi wachungaji kuhusu utaratibu wa kufungua na kuendesha ofisi.

## 6.6 KUMILIKI ARDHI

**Utangulizi**

Kufuatana na Katiba ya EAGT kila Kanisa liko "mahali", yaani liko juu ya kipande cha ardhi kilicho juu ya nchi (Mwanzo 1:10), chake au cha kukodi. Jengo laweza kuwa la kudumu au la muda, likiwa na hati ya kiwanja au bila kiwanja. Mungu aliumba ardhi kama chanzo cha chakula cha mwanadamu (Mwanzo 1:29-30). Lakini Yeye pia aliipanda bustani na kuchipusha mazao kutoka ardhi (Mwanzo 2:8-9), na Adamu alipewa wajibu wa kuilima na kuitunza (Mwanzo 2:15) hata kabla ya anguko la mwanadamu. Baada ya anguko ardhi ikalaaniwa na Adamu akaanza kula mazao ya ardhi kwa uchungu (Mwanzo 3:17b-18) na ikawa ni mahali pa kuweka mwili wake uliokuwa mavumbi. Baadaye Mungu akaweka utaratibu wa kuitumia kwa ajiri ya utajiri ila Anataka Mwanadamu asimsahau (Kumbukumbu 8:11-14 na 18). Adamu wa Pili ameleta upatanisho kati ya Mwanadamu na Mungu. Hivyo tuna haki ya kumdai

Shetani ardhi yetu na kumnyanganya kwa mamlaka tuliyopewa na Yesu (Luka 10:19) maana ilikuwa yetu na kuitakasa kwa damu ya Yesu Kristo.

Ardhi imebaki kama chanzo cha raslimali karibu zote muhimu ambazo mwanadamu hutegemea katika utajiri wake; maji, madini, mimea na mifugo. Ni kweli EAGT ina amini katika andiko la fedha ni mali yangu na dhahabu ni mali yangu, (Hagai 2:8), lakini uchambuzi wa mazingira umeonesha EAGT haijamiliki ardhi au maeneo ya kutosha kwa ajili ya maendeleo na Huduma za Jamii. Kama ilivyotajwa hapo juu ni vema kama sehemu ya kujenga hazina juhudi zifanyike kuwa na maeneo kwa ajili ya kufanyia huduma za Jamii, kujenga vyuo, maeneo ya makanisa ya kudumu na mikutano ya Injili.

**Lengo la 8**

**Ifikapo mwaka 2022 Makanisa mengi yawe yanamiliki maeneo makubwa ya Kanisa kwa ajili ya maendeleo na Huduma za Jamii.**

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Uongozi wa Jimbo uhamasishe wachungaji juu ya umuhimu wa KMP kumiliki ardhi.
ii. Mchungaji ahamasishe na kuwashirikisha waumini kuhusu umuhimu wa KMP na kila mshirika kumiliki ardhi.
iii. Mchungaji na viongozi wa KMP wajifahamishe sheria za nchi kuhusu umilki wa Ardhi.
iv. Eneo la Kanisa la Mahali Pamoja lipimwe na liwe na hati milki kufuatana na sheria za nchi.
v. Uongozi wa ngazi ya Jimbo uwe na eneo si chini ya ekari 10 kwa ajili ya kujenga ofisi, shule, maendeleo na huduma nyingine za Jamii.

## 6.7 KUMILIKI MAWASILIANO

**Utangulizi**

Kanisa la EAGT limekuwa na nia ya kuwa na vyombo vyake vya mawasiliano, lakini kusudi hilo lilichelewa kukamilika kwa sababu ya changamoto mbalimbali zikiwemo za raslimali fedha. Pamoja na hayo uchambuzi wa mazingira umeonesha wazi hitaji kubwa la kumiliki

vyombo vya habari kama Luninga, redio, magazeti na mitandao mingine. Uchambuzi umeonesha kuwa kuna fursa ya maendeleo ya technolojia ya mawasiliano, watu wana kiu na shauku ya Neno la Mungu inayoweza kutosherezwa na vyombo hivyo. Ikiwa watakuwa wanasikiliza redio au kutazama luninga na kusoma gazeti. Utaratibu pia wa kuanzisha vyombo vya habari siyo mrefu kama miaka 10 iliyopita.

Umuhimu mwingine wake ni kuwa vyombo vitachangia katika kuhubiri Injili na mafundisho, kupambana na maadili potofu pamoja na washirika wa EAGT kuwa na wachungaji wengi wa mitandaoni. Lakini pia faida ya kiuchambuzi yaonesha vyombo vya mawasiliano vitapambana na madhara ya utandawazi. Vyombo vya habari vitatumika kutoa mafundisho ya ujasiriamali, uongozi na elimu ya teolojia. Jinsi uwezo unavyoongezeka kanda zinaweza kuwa na vituo vya radio na hata Majimbo!

**Lengo la 9**

**Kumiliki vyombo vya habari ili kuwafikia watanzania wengi kwa neno la Mungu kwa urahisi zaidi**

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Kuamua ni asilimia ngapi ya hazina ya Taifa itumike kwa idara ya mawasiliano baada ya kukusanya sadaka za maendeleo.
ii. Kuajili mtaalamu mmoja wa awali mwenye fani ya tasnia ya habari kufuatilia kipaumbele cha mawasiliano.
iii. Mtaalamu wa Tasnia ya Habari kushauri Seckretariati namna ya kuanzisha idara ya mawasiliano EAGT.
iv. Kuchambua mazingira kuhusu fursa na changamoto za kuanzisha vyombo vya habari Tanzania (Gazeti, Radio na Luninga).
v. Kufuatilia utaratibu wa sheria za kuanzisha vyombo vya habari
vi. Kuhamasisha Kanda na Jimbo na Uongozi wa EAGT kuhusu umuhimu wa kumiliki chombo cha habari.
vii. Kuchambua na kutambua gharama za kuanzisha na kuendesha chombo hicho, Taifa na jimbo.
viii. Kutoa taarifa kwa wadau mbalimbali kuhusu maendeleo na mahitaji ya kuanzisha na kuendesha chombo.

# 7. MPANGO WA FEDHA

## 7.1 KUJENGA HAZINA

### Umuhimu wa kutunisha mfuko (Gharama ya Mshikamano)

Mshikamano ni gharama na kwa kipindi kirefu sasa EAGT imejikita zaidi katika kuhubiri Injili kuliko shughuli nyingine za Huduma ya Jamii, maendeleo na uchumi ya washirika si kwa pamoja. Jitihada zimefanyika za kununua shule ya Sekondari moja na kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu. Hili ni jambo jema lakini; kama Yesu alivyowalisha watu elfu tano (Yohana 6:10) baada ya mafundisho yake, sasa umefika wakati wa kutafsiri imani yetu katika matendo (Yakobo 1:27, 2:26; Mithali 19:17). Umoja wa EAGT lazima uonekana katika urithi wa pamoja pia. (Matendo ya Mitume 4:32) Mikakati ya kitaifa imeonesha umuhimu wa jambo hili (Angalia sura ya uchambuzi wa mazingira).

Uzoefu umeonesha kuwa nguvu za pamoja (Waefeso 3:4-5, Zaburi 133:1) na uwezo EAGT ilionao, ambao umeonekana katika uchambuzi wa mazingira yaani EAGT kuwa na mtandao wa makanisa mengi washirika haujavunwa ipasavyo. Kwa kiasi fulani hii inachangiwa na KMP kujiona liko pekee zaidi ya kuwa ndani ya umoja wa EAGT (Amosi 3:3, Mathayo 18:19). Sasa wakati umefika kujenga desturi ya "EAGT YETU" na "KANISA LANGU" kwa faida ya Habari Njema kwa wote.

Nafasi ya uhamasishaji na uelewa inahitajika kwa wachungaji na nidhamu ya kutimiza makubaliano ya michango, ahadi na sadaka za mshikamano. Mfano kama kila Kanisa lenye washirika kadhaa, kila mshirika atoe sadaka kiasi fulani ya Shule ya Jumapili itolewe shillingi kiasi fulani, na Mchungaji nae atoe shillingi kiasi fulani. Sadaka mbili, ile ya shule ya Jumapili na moja ya Mchungaji zitahusika kuimarisha Elimu ya Teolojia. Ya kwanza ni "Sadaka ya Mshikamano" ili kujenga Hazina ya Taifa na itawekwa kwenye "Akaunti ya Maendeleo". Ili ihusike na vipaumbele vya maendeleo. Sadaka nyingine ya Mchungaji ni kwa ajili ya uongozi na maendeleo. Wainjilisti na Walimu kuanzia ngazi ya Kanda na Taifa wajiunge. Kanisa zima kila baada mfano miezi mitatu, wiki ya mwisho sadaka inatolewa kwa ajili ya kipaumbele cha Injili na kuwasaidia wachungaji. Sadaka nyingine inatolewa na wataalamu na makundi maalum itaelekezwa kwenye shule za Seminari.

**Lengo la 10**

**Kuimarisha mshikamano na uwezo wa pamoja wa EAGT kifedha kwa ajili ya kufanikisha vipaumbele vya Kitaifa ifikapo mwaka 2021**

**Shughuli muhimu za kufikia Lengo**

i. Kuhamasisha na kutangaza kwa washirika vipaumbele vya kitaifa na nafasi yao katika utekelezaji wake. (Waebrania 13:16)
ii. Kuimarisha tabia na mwenendo wa kujitoa kwa ajili ya mshikamano wetu (Marko 11:25) sawasawa na moja ya nguzo zetu.
iii. Kuainisha kwa uwazi mchanganuo wa vipaumbele vinavyohitaji fedha, makusudi na wakati gani.
iv. Kukubaliana kila baada ya vipindi fulani vigezo vya kiwango cha kuchangia Hazina ya taifa.
v. Kujenga nidhamu ya Wachungaji katika kufuatilia na kutimiza makubaliano ya utoaji na ahadi (Kumbukumbu la Torati 23:23)
vi. Kufungua na kuendesha „Akaunti ya Maendeleo" na kujenga mfumo wa kifedha kutoka KMP hadi Taifa.
vii. Kuajiri Mhasibu ngazi ya shahada au mzoefu chini ya Mweka Hazina Mkuu au Mkurugenzi Mkuu (MM) ili kutunza mahesabu
viii. Kutambua kuwa fedha hizi zitakuja kama sadaka na si mapato ya Kanisa (Zaburi 20:3-5)
ix. Kuomba na kufunga kwa ajili ya roho ya hofu, kushindwa na kukosa utashi (Zaburi 34:4) na kujiamini (Wafilipi 4:13)
x. Kutoa taarifa ya maendeleo ya Ujenzi wa Hazina ya Taifa kila baada ya miezi minne kutumia vigezo vya makusanyo ya sadaka.
xi. Kuweka kigezo cha sadaka ya mshikamano ili kuwezesha Askofu na ofisi yake kupima maendeleo ya utendaji wa Jimbo na Kanda.
xii. Kila Jimbo na kila KMP liweke kujenga Hazina ya pamoja kama moja ya vipaumbele vyake.
xiii. Sadaka hizi zisitolewe kama jambo la ziada tu bali zipewe kipaumbele (Wafilipi 2:3).
xiv. Sadaka ya maendeleo kama itakayotolewa kama mara mbili kwa mwaka na Wachungaji wote, kadri Mungu atakavyowajalia. Wachungaji ni lazima (Matendo ya Mitume 4:34-37, 2 Wathesalonike 3:9).

## 7.2 MATUMIZI YA HAZINA YA TAIFA

### Lengo la 11

**Kutumia raslimali zitokanazo na hazina ya taifa kwa weledi na uaminifu sawasawa na mipango maalum iliyokubalika kuanzia Januari 2020.** (Mathayo 25:21)

Kama ilivyokwisha kuonesha EAGT imeanza kuwa na miradi ya kitaifa inayoendelea japo haijashika kasi sana; ikiwemo kuimarisha Chuo kikuu cha Taifa cha Teolojia Dodoma. Kwa wakati muafaka kipato kutokana na makao makuu -Dar-es-Salaam kitaongezwa kwenye sadaka ya maendeleo (Ujenzi wa makao makuu-Dodoma, seminari na mawasiliano). Uchambuzi wa mazingira umeonesha kuwa nafasi ya EAGT katika kutoa Huduma za jamii uko chini sana ikiwemo kutoyafikia makundi maalum (Yakobo 1:27, Mdo 6:1; Zaburi 68:5). Lakini pia makanisa yenye uwezo zaidi ya mengine yameendelea kwa kasi nzuri wakati kuna baadhi ya makanisa yenye shida. (Kumbukumbu la Torati 8: 12-14 na 8:18). Kwa hiyo matumizi ya Hazina ya Taifa yanalenga kushughulikia hayo mapungufu pia.

### Shughuli muhimu za kufikia lengo

- Kutengeneza mfumo na mwongozo wa kifedha wa namna ya kukusanya na kutumia fedha ya Hazina ya Taifa
- Kufungua akaunti ya Maendeleo ya Taifa itakayo pokea na kugawa raslimali hizo, chini ya Sekretariati au Mweka Hazina au Mkurugenzi wa Mipango na miradi.
- Kuajiri wataalamu (i) Mhasibu (ii) Mratibu ufuatiliaji na tathmini na (iii) Mratibu wa Miradi wa taifa na (iv) Afisa mawasiliano
- Kufanya maamuzi ya asilimia ya matumizi ya Hazina ya Taifa kila baada ya vipindi fulani
- Kutoa taarifa ya matumizi kila baada ya miezi sita kwa Halmashauri Kuu na au Kamati Kuu
- Kuteua kila KMP mtu mwenye roho wa Mungu (Mwanzo 41:38), mwaminifu na mwenye uwezo wa mali na kifedha, ili kuhusika na makusanyo.

- Kujenga uwezo wa Wakusanya sadaka, na kufanya makadirio ya makusanyo ngazi zote kufuatana na takwimu zilizopo za Wataalamu, Makundi maalum, washirika na wachungaji.

## 7.3 UTARATIBU WA MAKUSANYO YA SADAKA

Namna ya kuwasilisha na kuchangia sadaka ya Mshikamano (Maendeleo).

i. Mchungaji au Wazee wa Kanisa wasimamie uteuzi au uchaguzi wa mtunza makusanyo ya sadaka ya maendeleo, elimu ya teolojia uongozi na Injili.
ii. Mtunza sadaka awe na uwezo wa kusoma, kuhesabu na kuandika ngazi ya kidato cha nne au zaidi pale ambapo wanapatikana.
iii. Awe mshirika mwaminifu na asiwe ni mtu mwenye majukumu mengi tayari (kwa uzoefu wanawake ni watunzaji wazuri zaidi).
iv. Awe na simu inayoaminika na kwa maoni ya Mchungaji au wazee awe na unafuu wa kiuchumi (Mithali 30: 8-9).
v. Awajibike kwa upande wa sadaka ngazi ya Kanda au jinsi itakavyoelekezwa.
vi. Hata kama itapitia Jimboni mtu huyu mtunza makusanyo awajibike kwa Kanda
vii. Asiwe kati ya viongozi wa Jimbo, au Kanda kwa sababu ya wingi wa majukumu waliyo nayo tayari.
viii. KMP, Jimbo na Kanda Jimbo wawasimamie watunza makusanyo kwa njia hasa ya risiti au jumbe za mtandao.
ix. Mtunza makusanyo wa KMP na ngazi nyingine atumia fomu maalum kufanya makadirio na makusanyo jimbo na kanda watatumia fomu.

Maamuzi yatafanywa kila baada ya vipindi maalum kuhusu aina, kiwango na namna ya kutoa sadaka kutokana na uzoefu na mahitaji. Waraka kutoka ofisi ya Kamati Kuu utatumwa kote kuhusu viwango. Kwa hiyo makadirio ya sadaka zote yatafanywa na KMP, Jimbo, Kanda na Taifa. Makusanyo yatafanyika kufuatana na kipindi kilichoamuriwa. Halafu sekretariati itapitisha matumizi kufuatana na maombi au mahitaji. Baada ya matumizi taarifa itaandaliwa na kupelekwa kwa Kamati kuu, kabla (itakapokuwa lazima kupelekwa Halmashauri Kuu na hatimaye Baraza la waangalizi.

# 8. MPANGO WA UTEKELEZAJI

## 8.1 KIPINDI CHA MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI

Baada ya uzinduzi rasmi wa Mpango Mkakati tarehe 27 Juni 2019, Mpango unaanza na maandalizi kwa kipindi cha miezi sita, tangu 1 Julai 2019 hadi 31 Desemba 2019, au jinsi itakavyokubalika. Lengo la kipindi cha maandalizi ni kuhakikisha MMK-15 unasambaa nchi nzima na unaeleweka. Majukumu yanakuwa wazi, fomu za makusanyo na ufuatiliaji zinasambazwa na mafunzo yanafanyika. Ni wakati wa Viongozi ngazi zote kujizoeza Maono, Maadili 7 na nguzo 3, vipaumbele 7 vya miaka 15. Mikakati 12, malengo 12, matokeo 7 na hatua 12 za mpango Mkakati kufanikiwa. Viongozi pia wanahakikisha wakusanya sadaka wanafundishwa na fomu zinatosha na kutoa taarifa.

Ni fursa kwa KMP kumalizia mipango yao ili iendane na MMK-15 na Mipango ya Majimbo na Kanda. Fursa hii ni kwa ajili ya Uongozi kurekebisha kalenda zao za safari na vikao ili viingizwe kwenye mipango Kazi. Haina tija kufanya mambo yasiyokuwa katika Mpango Mkakati au Mpango wa Jimbo kwa sababu itavuruga matokeo ya baadaye na kuharibu mkataba. Undani wa kipindi cha maandalizi uko kwenye Mpango Kazi wa Jimbo na Kanda. Baada ya kipindi cha  kwanza cha miaka mitano kitaanza, kwa njia ya mpango kazi ambao utapangwa kwa undani wa miaka miwili ya kwanza. Namba moja ni mwezi wa kuanza kipindi cha maandalizi.

Ni muhimu kukawepo uwajibikaji mkubwa kwa viongozi wa Kanda, na kwa hiyo mwenye jukumu la kwanza la kuanzisha MMK-15 na Mipango Kazi ya Jimbo na Kanda na kusimamia, kuongoza na kufuatilia ni Maaskofu wa Kanda na Ofisi zao.

**Jedwali 3 Kalenda ya Kipindi cha Maandalizi**

| | KIPAUMBELE | MHUSIKA | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kusambaza MMK-15 | Baraza la Waangalizi | x | x | x | x | x | |
| 2 | Kuutangaza MMK-15 | Baraza la Waangalizi | x | x | x | x | x | |
| 3 | Kutangaza maono/ Maadili na vipaumbele | Baraza la Waangalizi | x | x | x | x | x | x |
| 3 | Kukamilisha MYM-3 | Uongozi wa Jimbo | | x | x | x | | |
| 4 | Kuitangaza MYM-3 | Uongozi wa Jimbo | | | | x | x | x |
| 5 | KMP kuandaa mipango | Wachungaji | | | x | x | x | x |
| 6 | Kukamilisha takwimu za Washirika | Wachungaji | x | x | x | x | | |
| 7 | Kuhamasisha sadaka ya Mshikamano, maendeleo nk | Wachungaji | | x | x | x | x | x |
| 8 | Vikao vya makundi maalum na wataalamu | Uongozi- Kanda na Majimbo | | | x | | | x |
| 9 | Kutekeleza mapendekezo | Kamati/Halmashauri Kuu | x | x | x | | | |
| 10 | Kufungua Akaunti ya Maendeleo | Mweka Hazina | | | | x | x | |
| 11 | Kuteua watunza sadaka wa KMP | Wachungaji | | | x | x | | |
| 12 | Kuwafundisha wakusanya sadaka | Mweka Hazina | | | | x | x | |
| 13 | Kufunga na kuomba-siku moja | Kamati kuu-wote | | | | | | x |

## 8.2 KALENDA YA MIAKA 15

Kalenda ya miaka 15 imewekwa kwa ujumla na undani wake utakuwa unarekebishwa baada ya tathmini, au kila mwaka katika vikao vya Halmashauri kufuatana na maarifa mapya.

**Jedwali 4 Kalenda ya vipaumbele miaka 15**

| KIPAUMBELE | LENGO NA | 2020-2024 | | | | | 2025-2029 | | | | | 2030-2034 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| Kuhubiri Injili | Nyumba kwa nyumba | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| | Mafunzo kwa Wainjilisti | | | x | | x | | x | | x | | x | | x | | x |
| | Mafunzo kwa wamissionari | | | | x | | x | | x | | x | | x | | x | |
| Ujenzi wa maofisi | Makao Makuu | | x | x | | | | | | | | | | | | |
| | Kanda | | | | x | x | x | | | | | | | | | |
| | Jimbo | | | | | x | x | x | | | | | | | | |
| | Mipango kazi-J | x | x | x | | | | | | | | | | | | |
| Mawasiliano | Utafiti | | | x | | x | | | | | | | | | | |
| | Eneo | | | | x | | x | | | | | | | | | |
| | Radio | | | | | x | x | x | x | | | | | | | |
| | Luninga | | | | | | x | x | x | x | x | | | | | |
| Kumiliki Ardhi | Kuwasiliana na ofisi za ardhi | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | | |
| | Kufuatilia maeneo | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| | Makadirio ya gharama | | | | x | x | x | | | | | | | | | |
| | Kulipia maeneo | | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | |
| | Kufuatilia hati miliki | | | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| Eli | Kuanza cheti | | | x | x | x | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| mu ya | Mitihani ya maarifa | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| Te | Matawi ya Chuo Kikuu | | | | | | | | x | x | x | x | x | x | x | x |
| olo Jia | Kuanza shahada ya 2 | | | | | | | | x | x | | | | | | |
| | Masomo ya walimu | | | | | x | x | x | x | x | x | | | | | |
| Hu du | Lishe ya watoto | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| ma | Shule za awali | | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| za | Shule za msingi | | | | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| Ja mii | Seminari za EAGT | | | | | | | x | x | x | x | x | x | x | x | x |
| | Tathmini MMK-15 | | | | | x | | | | | x | | | | | x |
| | Vikao vya Kurugenzi | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x |

## 8.3 MAJUKUMU YA KURUGENZI

### 8.3.1 Shughuli za kurugenzi

Katika utekelezaji; Kurugenzi zitakaa na kuchambua kwa undani majukumu yake. Lengo kuu la Kurugenzi katika MMK-15 ni; "kuwezesha na kusaidia Majimbo kufikia malengo yao katika kutekeleza mipango yao". Majukumu mengine ni kama ifuatavyo:-

i. Kuandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Idara ngazi ya Jimbo kwa kushirikiana na uongozi wa Jimbo kufuatana na malengo ya Jimbo.
ii. Kupokea mialiko au kuanzisha semina, warsha na kongamano kwa ajili ya kurugenzi kuendana na Vipaumbele 7 kutoka Majimboni.
iii. Kuandaa timu za wawezeshaji na waalimu wa maeneo mahsusi katika Mpango Kazi, ngazi ya Kanda kwa ajili ya kuwezesha majimbo, na hatimaye Majimbo ili kuwezesha KMP.
iv. Kuunda vigezo, maeneo mahsusi na mbinu za ushirikiano wa pamoja au muungano ngazi ya taifa na kuvitekeleza kitaifa kati ya kurugenzi zifuatazo: (i) WWI na CWI; (ii) WHI na VWI (iii) TEBE na KUSK. Ili muundo mpya na miongozo ianze kutumika mwaka 2021.

v. Kurugenzi kuwa na miongozo ya pamoja kufafanua na kushauri majimbo katika vipaumbele na malengo kama ifuatavyo: (i) Kuhubiri Injili- VWI/TEBE/KUSK; (ii) Huduma za Jamii-WWI/CWI; (iii) Kumiliki ardhi na mawasiliano-WHI (iv) Elimu ya Teolojia-KEM kwa kufuata Kalenda za majimbo na Kanda.

### 8.3.2 Muhtasari wa majukumu na mwelekeo

**Jedwali 5 Muhtasari wa majukumu ya Kurugenzi mwaka 2020**

| | KURUGENZI | KIPA UMBELE | MALEN GO | MWELEKEO |
|---|---|---|---|---|
| i. | TEBE, KUSK, (INJILI) | Kuhubiri injili | Lengo la 1 na shughuli zake | Ziongoze maendeleo ya Injili, kupitia semina na mafunzo maalum |
| ii. | CGM (VWI) | Kuhubiri injili Huduma za jamii | Lengo la 2, na shughuli zake | Maendeleo ya Vijana walio pia vyuoni na sekondari. Semina na mafunzo maalum |
| iii. | ELIMU NA MAFUNZO (KEM) | Kuimarisha uongozi, na Elimu ya teolojia | Lengo la 3,4 na Shughuli zake | Wajikite pia kwenye maendeleo ya Wachungaji na elimu ya EAGT, na mafunzo maalum kwa Wachungaji |
| iv. | WWI, CWI | Huduma za jamii | Lengo la 5 na 6 | Maendeleo ya Wanawake na watoto. Semina na mafunzo maalum kwa wanawake na watoto |
| v. | WHI | Ardhi na mawasiliano | Lengo la 7,8, 10 | Maendeleo ya wanaume, ardhi, mawasiliano na kuwekeza. Semina na mafunzo maalum |

## 8.4 MAJUKUMU YA KANDA

Uongozi wa Kanda katika utekelezaji wa MMK-15 na Mipango ya Majimbo ni kufanikisha kipaumbele na malengo yanayohusu;

“Kuimarisha Uongozi” ndani ya Kanda nzima. Kufuatilia taarifa na kufanya maamuzi baada ya kupokea takwimu zinazotoka Majimboni kila miezi minne. Uongozi wa Kanda utachambua chanzo cha mafanikio au changamoto Majimboni na kuzifanyia kazi. Uongozi wa Kanda utashirikiana na Kamati Kuu-EAGT kuimarisha viongozi ngazi zote katika Kanda nzima. Kuongoza au kujipanga upya kuhusu sadaka za mshikamano yaani; Injili, elimu ya teolojia, uongozi na maendeleo. Kanda zitaendelea kuwa kiunganishi muhimu kati ya Kamati Kuu na Majimbo, kwa hiyo mafanikio ya mipango ndani ya EAGT yataongozwa na Kanda chini ya uangalizi wa Kamati Kuu!

## 8.5 MUUNDO WA UTEKELEZAJI MMK-15

### 8.5.1 Umuhimu wa muundo unaoendana na MMK-15-KMP

Baada ya Mkakati mpya ni lazima EAGT iwe na muundo mpya wa utendaji au muundo uliopo uboreshwe kulingana na maono, vipaumbele, maadili ya msingi na malengo ya miaka 15. Ili kutekeleza shughuli za kila siku kwa ufanisi na kwa vipindi vilivyopangwa kwa ajili ya kuvuna matokeo yanayotarajiwa, muundo mpya ni muhimu sana. EAGT ikibaki na Muundo wa utendaji ule ule kabla ya Mpango Mkakati na raslimali watu ile ile, yenye utendaji ule ule, EAGT isitarajie matokeo tofauti! Kwa hiyo muundo wa utendaji pendekezwa ni kufuatana na vipaumbele, mkazo ukiwekwa ngazi ya KMP, Jimbo na Kanda.

### 8.5.2 Kanisa la Mahali Pamoja

i. Hakuna mabadiliko, isipokuwa KMP liandae Mpango Kazi wake pamoja au shughuli kuendana na shughuli zilizotajwa kwenye Mpango Kazi wa Jimbo na Kanda, hasa zile ambazo ni maalum kwa ajili ya KMP, ikizingatia takwimu za washirika wake.

ii. Mchungaji ni Kiongozi wa KMP. Muundo wa Wazee wa Kanisa na Mashemasi unabakia ule ule kama ilivyo kwenye Katiba ya 2011. Kama ni lazima ingefaa majukumu yao yarekebishwe kufuatana na vipaumbele vya kitaifa na Mpango Kazi wa Jimbo na Kanda.

iii. Idara zote ziendelee, inapendekezwa WHI ichukue wanaume wote waliokwishaoa. CGM iitwe VWI-Vijana wa Huduma ya Injili,

iwe na vijana wavulana na mabinti ambao hawajaoa kuanzia miaka 16, kama sera ya Tanzania kuhusu vijana ilivyo. Ushirikiano wa karibu kati ya WWI na CWI uanzishwe ikibidi kiongozi wa idara KMP hizi awe mmoja, inafaa pia Kiongozi (Mwenyekiti) wa VWI awe kijana pia. TEBE na KUSK zishirikiane au ziunganishwe. Kila mshirika na awe katika Idara moja. Kanisa changa lisilazimike kuwa na idara zote nane.

### 8.5.3 Mgawano wa majukumu kwa vipaumbele- Jimbo

Muundo unaopendekezwa ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi ili Jimbo litekeleze Mpango kazi kutokana na MMK-15. Kama kila Kurugenzi ina watu 4, na kama zote zipo Jimboni, hii ni sawa na viongozi 32, ukiongeza na viongozi wa Jimbo 4, hii sawa na viongozi 36. Na kama Kanda inao 36 japo ni kwa Makanisa yote, ni wazi viongozi ni wengi. Kama kuendesha ofisi hizi kunategemea KMP, wingi wa viongozi hawa hautaleta ufanisi kwa Mpango Kazi. Hivyo lazima kuunda timu ndogo ya kuratibu na kushauri makanisa ya MP kuendana na vipaumbele saba. Uongozi unahitaji kutenda kama timu, japo kila nafasi ina majukumu mahususi**.** Majukumu yafuatayo yanaangukia katika vipaumbele.

**Kuhubiri Injili:-** Inahusu uratibu na usimamizi wa Injili Jimboni, maendeleo yake na ya vijana. Mratibu wa kipaumbele cha Kuhubiri Injili awe Mchungaji lakini kijana na mwenye nguvu bado (miaka 30-45). Mwenye huduma ya Uinjilisti, awe na Stashahada kutoka Chuo cha EAGT au Shahada.

**Kuimarisha uongozi:** Inahusu usimamizi, utetezi, kulinda Imani ya EAGT na misingi yake katika Jimbo na nidhamu ya watumishi wa Mungu Jimboni. Kusimamia maono ya EAGT, dhima na maadili 7 ya msingi na kuiwakilisha EAGT katika Jimbo. Mratibu ajue kusoma na kuandika angalao elimu ya msingi. Ahudhurie masomo ya muda mfupi ya uongozi kwenye Chuo cha EAGT.

**Elimu ya Teolojia:** Inahusu uratibu wa shughuli zote za waalimu wa Neno la Mungu Jimboni na waalimu wa shule ya Jumapili. Uhamasishaji, kufuatilia Wachungaji wajielimishe (QT) na kwenda Vyuo vya Teolojia. Uimarishaji wa uhusiano wa Jimbo na Chuo cha Kanda-na Chuo Kikuu. Uratibu wa masomo na semina za waalimu na wainjilisti.

Kutangaza Vyuo vya EAGT katika Jimbo kwa watu wote akianzia makanisani, halafu madhehebu mengine na watu wote. Itafaa sana mwenye kuratibu hiki kipaumbele awe na Stashahada na baadaye shahada kama hana.

**Huduma za Jamii:-** Ziko huduma za Jamii ndani na nje ya Kanisa. Jukumu ni kuratibu Shule za awali, na za Msingi Jimboni na walimu wao, shughuli za maendeleo ya wanawake na watoto na lishe ya watoto makanisani. Kushauri ujenzi wa shule za Msingi makanisani au hata Jimbo, na wataalamu na makundi maalamu Jimboni. Ni kiungo katika ujenzi wa Seminari za EAGT za Kanda-. Ingefaa mtaalamu Mwalimu akaribishwe kuratibu eneo hili.


**Kumilki ardhi:** Hii inahusu uratibu wa shughuli za kumiliki ardhi, viwanja, mashamba, ujenzi wa makanisa ya kudumu na hati milki. Ufuatiliaji wa sheria za ardhi na kushauri makanisa, kuratibu na kushauri uanzishwaji wa miradi ya KMP na shughuli nyingine za maendeleo ya WHI katika Jimbo. Akishirikiana na kuwasiliana na Wadhamini kabla ya maamuzi ya mwisho kuhusu ardhi. Haya majukumu yangefaa apewe mtu kutoka makundi maalumu kama mfanya biashara**.**

**Mawasiliano:** Hii ni juu ya uratibu wa mfumo mzima wa ukusanyaji, kutunza, kuhakiki na kuchambua takwimu muhimu za Jimbo kufuatana na viashiria. Kutoa taarifa kwa kipindi kilichopangwa kwa ajili ya ufuatiliaji, kupima na kutathmini utekelezaji wa MMK-15, na utendaji wa shughuli za kufikia malengo ya Jimbo. Kuhakikisha fomu zote zinazohusu KMP zinawafikia wakusanyaji sadaka na ufuatiliaji. Kuwakilisha Jimbo katika kumiliki vyombo vya mawasiliano. Hii ingefaa apewe mwenye ujuzi au utayari wa kujifunza komputa. Kuhusika na utunzaji wa taarifa/takwimu za sadaka za mshikamano kutoka KMP, kuziandaa na kuziwasilisha. Kushiriki kujenga uwezo wa Wakusanya sadaka za Injili, Maendeleo, Teolojia na Uongozi.

**Ujenzi wa Maofisi**: Usimamizi na uratibu wa shughuli za raslimali na mali za Jimbo. Kutunza mapato ya Jimbo yatakayotokana na kumbi, miradi, mashamba au uwekezaji. Kusimamia ujenzi wa ofisi ya Jimbo na KMP (kuunganisha wahandisi wa Jimbo), ni kiungo katika kuratibu Ujenzi wa ofisi ya Kanda.

Uongozi wa Kanda utafanya kazi na Kamati Kuu na kuhakikisha MMK-15 unafanikiwa na kuamua mahitaji ya Uongozi jimboni. Jimbo linaweza kuanza na mtu mmoja na baadae wawili halafu watatu.

### 8.5.4 Mchoro wa muundo ngazi ya Taifa




### 8.5.5 Majukumu ya Sekretariati

i. Kuchagua na kusimamia waajiriwa wa EAGT kufuatana na sheria za Nchi
ii. Kuratibu shughuli za wataalamu na makundi maalum kupitia timu za Majimbo na Kanda
iii. Kufuatilia sera, miongozo na sheria za nchi kuhusu Elimu, ardhi, mawasiliano na Huduma za Jamii nk
iv. Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji, na tathmini ya vipaumbele vya EAGT vya miaka mitano ya kwanza
v. Kuratibu mipango ya maendeleo ya Kanisa la EAGT
vi. Kupokea taarifa za makadirio na makusanyo ya sadaka zote kutoka nchi nzima
vii. Kusimamia mipango, na matumizi ya vipaumbele kama ilivyopitishwa na Halmashauri kuu
viii. Kupendekeza viwango vipya vya sadaka kwa Kamati kuu na hatimaye Halmashauri kuu na Baraza la waangalizi
ix. Kusaidia bodi na Kamati zilizomo ndani ya EAGT na Wadhamini kufanya maamuzi endapo itaombwa kufanya hivyo.

Sekretariati itawajibika kwa Kamati Kuu na kutekeleza maamuzi ya Halmashauri Kuu. Inapendekezwa Sekretariati kudumu kwa miaka mitatu. Wajumbe wateuliwe na Kamati Kuu kufuatana na sifa maalum. Italazimu kuwe na kipindi cha mpito kati ya miezi 6 hadi mwaka.

#### 8.5.6 Wajumbe wa Sekretariati

Wajumbe wawe kati ya 9-12, wanaweza kujiunda katika timu ndogo ndogo za watatu, wanne au hata wawili nao ni:
(i) Mtaalamu wa Elimu (ii) Mwanasheria, (iii) Maendeleo ya Wanawake (iv) Maendeleo ya watoto (v) Maendeleo ya ardhi (vi) Maendeleo ya Injili (vii) Maendeleo ya Wachungaji (viii) Wataalam/Kundi Maalum (ix) Maendeleo ya Vijana (x) Maendeleo ya Mawasiliano (xi) Katibu (xii) Mkurugenzi.

## 9. MPANGO WA UFUATILIAJI

### 9.1 TAKWIMU MUHIMU

Kama ilivyotajwa hapo juu EAGT inakabiliwa na changamoto ya kutunza kumbukumbu (Mat 10:30, Ezra 2:1-58, 1Nya 27:1-15) sahihi na endelevu Hes 1 na 26. Ni muhimu kujua kuwa uongozi na utawala unahitaji maamuzi yenye takwimu. Ni vigumu sana kupanga, kupima, kutathmini maendeleo ya EAGT bila takwimu kwa ngazi zote. Kukosa mfumo mzima wa Kanisa wa ufuatiliaji ni sehemu ya kitisho. Mikakati imependekezwa ya kushughulikia mapungufu hayo. Maamuzi ya Kanisa sasa lazima kila inapobidi yaendane na takwimu zilizopo. Kila Jimbo liwe na takwimu zake kutokana na takwimu za KMP. Maamuzi ya Kiongozi bila takwimu ni sawa na kufungua macho kwenye giza nene!

**Lengo la 12**

**Kuandaa na kuboresha mfumo wa taarifa na ufuatiliaji wa EAGT ifikapo 2020**

**Shughuli muhimu za kufikia lengo**

i. Kila Kanisa lazima liwe na takwimu za kila mshirika kwa kujaza fomu maalum au kufungua daftari (Idara zihusike kikamilifu) (Luka 2:2-4)
ii. Kila mtoto anayebarikiwa ajaziwe takwimu zake na Kanisa la Mahali Pamoja (Luka 2:22)
iii. Kila Kanisa liwe na makundi yafuatayo ya washirika, chini ya mwaka mmoja, chini ya miaka mitano, kati ya 6 na 14, 15 hadi 35 na zaidi ya hapo (watu wazima.
iv. Kila baada ya kipindi maalum kama miezi minne, takwimu zirekebishwe ili kuona washirika wapya waliohama au kuhamia, kuokoka au kurudi nyuma au hata kufariki.
v. Kila Mchungaji ajaze fomu ya „Hojaji ya Mchungaji" na kila Katibu wa Jimbo atafanya majumuisho na kutunza takwimu hizo. Kanda na Taifa zitafanya hivyo hivyo.
vi. Kila mchungaji atapewa namba ya Jimbo na kufunguliwa jalada ili takwimu zake ziwekwe na Ofisi ya Askofu wa Jimbo.
vii. Waalimu na wainjilisti takwimu zao zitunzwe kwenye Ofisi ya Kanisa la Mahali pamoja wanakoabudu.
viii. Kila jimbo litengeneze kanuni ndogo ndogo zisizozidi 3, ili kuwasaidia katika mipango ya Jimbo, vikao, zaka, vipaumbele vya Jimbo na Taifa na taarifa za kila baada ya miezi sita na mwaka.
ix. Idadi zote zilizo kwenye Jedwali ya Jimbo zijulikane na ziwe zinatumika katika mipango na vikao vyote vya Jimbo.
x. Jimbo liwe na mtu mmoja atakaye husika na ufuatiliaji na tathmini kufuatana na Jimbo lilivyo jipangia (au kati ya wale viongozi wanne).
xi. Kila Mchungaji awe na Msaidizi (au yeye mwenyewe) atakaye fuatilia eneo hili muhimu la takwimu. Ikiwezekana awe ni mtaalamu au amemaliza Kidato cha 4-6 na kuendelea, ikiwezekana ajue komputa (mjini).
xii. Ngazi ya Kanda pia wawe na mtu mmoja atakaye husika na eneo hili la ufuatiliaji na tathmini. Sifa ni zile zile au mmoja kati ya viongozi wanne.

## 9.2 MATOKEO YA MMK-15

### 9.2.1 Matokeo ya miaka 15

**Utangulizi**

Mpango Mkakati lazima uambatane na Mpango wa tathmini na ufuatiliaji. Takwimu za awali zimetokana na takwimu za Kanisa, Hojaji ya Mchungaji na takwimu ya Jimbo na mshirika. Ili kuweza kufuatilia mafanikio ya Mpango Mkakati na Mipango wa Jimbo, vigezo 12 au viashiria vimepangwa. Kila baada ya kipindi cha Miezi minne takwimu zitakusanywa na taarifa kupelekwa ngazi ya Jimbo, Kanda na Taifa jinsi itakavyohitajika, ili kufuatilia matokeo na utendaji.

Matokeo ni matunda (Marko 4:8) ya shughuli na malengo mbalimbali ikiwemo raslimali watu, muda na fedha. Maandiko yanatutaka tuamini, (Waebrania 11:1, Luka 1:37, Wafilipi 4:13). Matokeo 7 yaliyo katika Mpango Mkakati yanahusiana na vipaumbele. Maana yake ukitekeleza vipaumbele utapata nini? Tunaamini yote haya yatapatikana hata zaidi.

i. Miaka 12 ijayo washirika wataongezeka mara nne zaidi ya sasa na asilimia 50 ya makanisa yatakuwa na majengo ya kudumu, yakimiliki ardhi eka 2 na zaidi.
ii. Baada ya miaka 10 asilimia 50 ya Wachungaji watakuwa na shahada ya Elimu ya Teolojia. (Mithali 9:9; 8:33)
iii. Asilimia 75 ya watoto wanaozaliwa sasa watakuwa kidato cha kwanza au na shule za ufundi baada ya miaka 15.
iv. EAGT itakuwa na Chuo kikuu cha Teolojia chenye matawi katika Kanda 5 ifikapo miaka saba. (Mithali 23:12)
v. Kila Kanda itakuwa na Seminari kiwango cha sekondari na au shule ya Msingi kuanzia miaka saba ijayo.
vi. Kila Kanda na kila Jimbo litakuwa na ofisi ya kudumu (muhuri, akaunti, utunzaji wa kumbukumbu mwishoni mwa miaka 12, na kitega uchumi kimoja au zaidi.
vii. Kati ya miaka 10 na 15, Luninga au Radio EAGT ya Habari Njema itakuwa hewani kwenye asilimia 25 ya maeneo ya Kanda.

### 9.2.2 Maelezo ya Matokeo

i. Injili iliyo hai itahubiriwa, washirika kuongezeka, makanisa yataweza kufanya huduma za Jamii zenye viwango na hivyo yanahitaji majengo ya Kanisa ya kudumu na kumiliki maeneo ya ardhi kwa shughuli za miradi, kumbi hostel nk.
ii. Mchungaji mwenye kumaliza darasa la saba achukue mwaka kujiandaa, halafu mitatu ya kufanya QT (Mtihani wa Maarifa), miaka miwili asome stashahada, awe na mwaka wa mapumziko na mitatu asome shahada ya Theolojia hii ni sawa na jumla miaka 10.
iii. Shule za awali zitaanzishwa katika makanisa mengi, hivyo watoto watapata mwanzo na maandalizi mazuri kwa ajili ya kuanza shule ya msingi.
iv. Watoto chini ya miaka 5 watakuwa na lishe bora na kuwa wenye afya nzuri, hivyo kufuatilia masomo ya msingi kwa wepesi.
v. Kanda mbili au kila kanda pekee itakuwa na shule ya Msingi ya au Seminari za EAGT, kwa maana itapokea wanafunzi kutoka kanda zote bila kujali Kanda, hizi zitaendelea kuwa sekondari.
vi. Ujenzi wa Chuo Kikuu unaendelea, na ili kuondoa msongamano wa masomo baada ya miaka 5 Vyuo vya Kanda vitakuwa vimeimarika na hivyo kuweza kuwa na stashahada au cheti ya matawi ya Chuo Kikuu cha Teolojia. Vyuo vitawekea mkazo masomo ya Uinjilisti, Umisheni, Ualimu, Uongozi na utawala.
vii. Utunzaji wa kumbukumbu umeishaelezwa, kila kanda itakuwa na sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu za wachungaji, Waalimu, Wainjilisti, n.k, kusaidia ufuatiliaji wa mambo kama ya sera za serikali, sheria, hati miliki, hata kumbi kama vitega uchumi.

Kwa ujumla wake vipaumbele vitategemea jinsi EAGT nzima itakavyoshiriki katika kuchangia ujenzi wa hazina ya taifa na kuwa tayari kutoa sadaka ya mshikamano. Vyanzo vya mapato kama kumbi uwekezaji (hisa) vitabuniwa baada ya kuwa na mtaji wa awali kutoka Hazina ya Taifa.

## 9.3 TAARIFA ZA MIEZI MINNE NA MWAKA

### 9.3.1 Viashiria-vigezo Muhimu kwa Jimbo

Inawezekana Jimbo kuwa na viashiria vingi, lakini vimechaguliwa 12 tu, ambavyo pia vitatumika ngazi zote.

**Jedwali 6 Viashiria vya fuatilia utendaji**

| | **ENEO LA KIASHIRIA-MIEZI 4X3** | **MAELEZO** |
|---|---|---|
| i. | Jumla ya matawi mapya yaliyofunguliwa Jimboni | Jumlisha Idadi ya matawi kutoka kila Kanisa kwa miezi minne |
| ii. | Idadi ya washirika wapya waliojaziwa fomu au kuokoka | Jumlisha washirika wapya kutoka kila Kanisa kwa Jimbo zima kila miezi minne |
| iii. | Idadi ya watoto waliozaliwa | Jumlisha watoto wote waliozaliwa ndani ya miezi minne |
| iv. | Namba ya mikutano mikubwa ya Injili kwa mwaka | Jumlisha mikutano yote Jimboni gawanya kwa idadi ya makanisa |
| v. | Namba (asilimia)ya makanisa yaliyoanzisha shule za awali | Jumlisha makanisa yote yenye watoto zaidi ya 20 (K) walio chini ya mwaka 1. Hesabu makanisa mangapi kati ya haya yameanzisha shule (A). Gawanya (A) kwa (K) na zidisha mara 100 |
| vi. | Namba ya makanisa yenye utaratibu wa (lishe) kunywa uji-watoto chini ya miaka 5. | Hesabu makanisa yote yenye utaratibu wa kuboresha lishe ya watoto chini ya miaka 5 (A). Gawanya kwa makanisa yote (K) zidisha mara 100 |
| vii. | Namba ya makanisa yaliyotuma Kanda sadaka ya maendeleo | Jumlisha makanisa yaliyotuma sadaka ya maendeleo yote (A) kwa mwezi. Gawanya kwa makanisa yote ya Jimbo (B) zidisha mara 100. Jumlisha asilimia zote za miezi minne, halafu gawanya kwa nne kupata wastani. |
| viii. | Idadi ya wachungaji waliotuma sadaka yao ya Elimu ya teolojia | Jumlisha wachungaji wote waliotoa sadaka kwa miezi vinne (A). Zidisha mara 4 wachungaji wote (B). Gawanya |

| | | |
|---|---|---|
| | | A kwa B, halafu zidisha mara 100 |
| ix. | Idadi ya Makanisa yaliyo pata eneo eka 2-5 na zaidi yenye hati | Hesabu makanisa yaliyopata eneo eka 2-5, (A) gawanya kwa makanisa yote (B) zidisha mara 100 |
| x. | Idadi ya makanisa yenye mipango au malengo | Jumlisha makanisa yote yenye mipango (A) gawanya kwa makanisa yote (B) halafu zidisha mara 100 |
| xi. | Idadi ya makanisa yaliyoanzisha SACCOS | Jumlisha makanisa yote yenye SACCOS (A) gawanya kwa makanisa yote (B), halafu zidisha mara 100 |
| xii. | Makanisa yaliyoanza miradi ya kanisa | Jumlisha makanisa yote yaliyoanzisha miradi (A) gawanya kwa makanisa yote Jimboni (B) zidisha mara 100 |

Fomu zimeandaliwa na zitaanzia kwa Kanisa la Mahali Pamoja kutokana na viashiria vya hapo juu.

### 9.3.2 Kutoa taarifa na kupanga kila mwaka

Jimbo litakusanya taarifa zake kufuatana na viashiria kila baada ya miezi minne au jinsi litakavyoamua. Baada ya miezi minne kuisha, Jimbo lipeleke taarifa za miezi minne kwenye ofisi ya Kanda zikiambatana na maelezo mafupi. Yaani uchambuzi wa Jimbo. Kanda ipokee taarifa za mwaka mzima kwa kutumia viashiria vilivyowekwa katika fomu za ufuatiliaji. (Angalia kitabu cha mpango kazi fomu na 13- 17). Kila baada ya mwaka mmoja (au miezi minane) Jimbo na Kanda wakae kujadili taarifa ya viashiria vyao na kufanya maamuzi kuhusu maendeleo ya Kanda na Majimbo ili kujipanga tena kwa mwaka mpya unaofuata. Tathmini ya kina itafanyika baada ya miaka 3-4 ili kuboresha dira ya miaka mitano inayofuata.

## 9.4 VIGEZO ILI KUFANIKISHA MMK-15 NA MIPANGO

Ili MMK-15 na Mipango mingine ifanikiwe lazima viwepo vigezo, mazingira rafiki na masharti ya kufuatwa au mambo ya lazima kutendeka (Isaya 1:19). Wengine huita hii kama „Mpango wa kujihami‟ au vipengele vya kufanikiwa. Ambavyo visipokamilishwa MMK-15 mzima huharibika. Yaani matokeo yaliyotarajiwa hayatafikiwa na

malengo hushindikana. Jedwali na 16 linaonesha maeneo 7 muhimu na ya lazima, ikiaminika kuwa EAGT inaishi maadili 7 ya msingi.

**Jedwali 7 Vigezo vya lazima ili MMK-15 na Mipango ifanikiwe**

| | KIPENGELE | HATUA ZA LAZIMA |
|---|---|---|
| I | Upatikanaji wa raslimali fedha | i. Kila mshirika kutoa sadaka ya kujenga Hazina ya Taifa kwa wakati muafaka<br>ii. Wachungaji kusimamia na kuhamasisha kwa uaminifu utoaji wa sadaka mbalimbali<br>iii. Mtunza Makusanyo kuwa mwaminifu na kuwasilisha makusanyo kwa wakati<br>iv. Wachungaji kuthamini na kuwa na mtazamo wa Umoja wa EAGT badala ya kubakia KMP tu (Mdo 4:32) |
| II | Elimu ya teolojia | v. Makusanyo ya sadaka kutoka kwa matoleo ya Shule ya Jumapili kuwasilishwa kwa wakati<br>vi. Wachungaji kutoa sadaka zao za Elimu ya teolojia ya uongozi kwa wakati |
| III | Majukumu mengi kwa mtumishi mmoja | vii. Halmashauri na Kamati Kuu kuhakikisha kuwa kuna mgawano mzuri wa majukumu (Kutoka 18:19) kwa ajili ya ufanisi na afya za Watumishi |
| IV | Ufanisi katika kutoa taarifa | viii. Uongozi ngazi zote kukusanya takwimu, kutoa taarifa kwa wakati na kufanya maamuzi kwa kutumia viashiria/takwimu |
| V | Uongozi imara na utawala makini | ix. Viongozi kuonesha njia katika utekelezaji wa MMK-15 na mipango iliyomo katika MMK-15.<br>x. Kubadili mitazamo, msimamo na kujenga mitazamo mipya (Luka 5:37-38), katika kufuata mipango na shughuli zilizopangwa |
| VI | Mpango ni Mkataba | xi. Viongozi kutambua kuwa Mpango ni mkataba kati ya washirika na viongozi wao, na kutoufuata na kuuvunja ni |

| | | |
|---|---|---|
| | | kutotimiza ahadi (Kumbukumbu la Torati 23:23) |
| VII | Viongozi kuwa mfano | xii. Mwenendo wa viongozi kuwa mfano wa kuigwa, kwa kuamini wanayo hubiri na kufundisha, katika kuziishi nguzo („Utakatifu‟, „Uongozi‟ na „Utoaji‟), kusimamia na kufundisha Maadili 7 ya Msingi (Mathayo 5:15, 2Wakorintho 6:3-4) |

## 10. WASHIRIKI KATIKA MCHAKATO WA KUANDAA MMK

| KAMATI KUU | |
|---|---|
| Askofu Mkuu | Rev. Dkt. Brown Mwakipesile |
| Katibu Mkuu | Rev. Dkt. Leonard Mwizarubi |
| Mweka Hazina Mkuu | Rev. Dkt. PrayGod Mgonja |

| **Kanda ya Nyanda za juu Kusini kati** | **Kanda ya Ziwa Rukwa** | **Kanda ya Kati** |
|---|---|---|
| Rev Simon Mwakaliko | Rev Silvester Msumeno | Rev. L. Denis |
| Rev. Patrick Mbao | Rev. N .J. Mwanisawa | Rev. Ibrahim Kiula |
| Rev. Emmanuel Kitundu | Rev. Henry .T. Chomola | Rev. J Mafwimbo |
| Rev. Aradini Mwangomba | Rev. A.L. Mwakatumbula | Rev. Mussa Maselo |
| Rev. Madaraka Ndenjela | Rev. Nimeona Kaboneka | Rev .Wilison Mkoma |
| Rev. Jailo Mwaseba | Rev. Marko .E. Kauzeni | Rev. W. Samson |
| Rev. Aloys Marwa | Rev.Sixtus .J. Mikoma | Rev. S. Ogenga |
| Rev. Amos .B. Ngonyani | Rev.P Mbalamwezi | Rev. Ignas George |
| Rev. Eliya .W.Simbeye | Rev. L. Masoud | Rev. Partson Wiliam |
| Rev. Camily Athanase | Rev.Venance Moche | Rev. Simon Luhanga |
| Rev. A. Mwakatago | Rev. Amry Songoro | Rev. Joseph Enock |
| Rev. S. H. Goliama | Rev. D. K. Mbaga | Rev. David Kimani |
| Rev. Obed .R. Cheyo | Rev.N.F. Mwanandeje | Rev.Jacob Dandi |
| Rev. Akimu Mwanyilu | Rev. Julius .K. Shapanga | Rev. Gerald Mhinga |
| Rev. E .M. Mwambonake | Rev.Oscar .A. Simbeye | Rev. S. Nyangalima |
| Rev. Wisdom .M. Gowele | Rev. Elias Swata | Rev. G. Lukinga |
| Rev. Eliah .W. Membe | Rev. Simon Kitwika | Rev. G. Maniyangulu |
| Rev. E .F. Mwaitwalile | Rev. Simon T Kitwila | Rev. V.R. Mhumba |
| Rev. J. Mwambwagilo | Rev. Angelus T. Milinga | Rev. Barnabas John |
| Rev. Peter Nzunda | Rev. Emmanuel Ketundu | Rev. Peter .J. Oballa |
| Rev. Lodrick Ngendwa | Rev. Bavoti Isaya | Rev. Moses Chihoma |
| Rev. Uswege Mwakafwila | Rev. Daudi K. Mbaga | Rev. Julius Kimonga |
| Rev. Edward Kapokola | Rev. Obadia Zakaria | Rev. M. S. Sweddy |
| Rev. Tedy Ndenjela | Rev. Dkt. Joshua Wawa | Rev. Barnabas John |
| Rev. Asumsie Lwesya | | Rev. Victor Salulo |
| Rev. Ande Mwakyambiki | | Rev. D.Majeranga? |
| | | Rev. J. T. Nassary |

| Kanda Ya Magharibi | Kanda Ya Ziwa Magharibi | Kanda Ya Ziwa Mashariki |
|---|---|---|
| Rev. Stephen Mloy | Rev. R. Machimu | Rev. George Gecha |
| Rev. A. Kadelema | Rev. John Okongó | Rev. Lameck Nkumba |
| Rev. Peter Madaha | Rev. Winifrida James | Rev. Gregory Kapela |
| Rev. Alex Kinyamgala | Rev. Batrolomayo | Rev. Richard Kapalaswa |
| Rev. Yohana Jarome | Rev. D.S. Masembo | Rev. Paul .A. Nyanda |
| Rev. Isaack Nchunga | Rev. John Mpuya | Rev. Simon Ndegeiswa |
| Rev. Josephat Kilibaze | Rev. Nixon .R. Feruzi | Rev. Cosmas Shimbe |
| Rev. Josias .M. Gwemela | Rev. Charles Paul | Rev. Daniel Malibata |
| Rev. Fanuel Daniel | Rev. J. Lutego | Rev. Thomas Lyoba |
| Rev. Joshua Zacharia | Rev. Zacharia Seni | Rev. Lukas Luhende |
| Rev. Joshua Nayingo | Rev. E. Magezi | Rev. Amon Lutelemla |
| Rev. Festo Njige | Rev. Rutha Mbagwa | Rev. Aaron .M. Mlewa |
| Rev. Emmanuel Philipo | Rev. M..E. Ngule | Rev. Saimon Mahuna |
| Rev. Marko .M. Mponda | Rev. E. Bubinza | Ms. Monica Mbaraka |
| Rev. Gideon .J. Bushize | Rev. E. Kaselya | Mrs. Specioza Jokakuu |
| Rev. Yusufu .Y. Mbanza | Rev. L. Kabakaki | Mrs. Beatrice Mgonja |
| Rev. Peter Mwinamila | Rev. J. Mbagwa | Dkt. A.L. Mwizalubi |
| Rev. Joshua Zacharia | Rev. Paulo Bonifasi | Rev. Sebastian .I. Bwiri |
| Rev. P. W. Mwananjela | | Rev. E.I .L. Kamalamo |
| Rev. Alfred K. Kapwacha | | Rev. Dkt. L.M. Sefania |
| | | Rev. Joshua Maswi |
| | | Rev. R. P. Kapaliswa |

| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mashariki | | |
|---|---|---|
| Rev. Raphael Kayombo | | |
| Rev. Alfed Mwagike | Rev.N.R. Msigwa | Rev. Nico Mpogolo |
| Rev. Michael Kilasi | Rev. F. Mapunda | Rev. Ezekiel Mwenda |
| Rev. Nodhrey Sanga | Rev. A.T. Millinga | Rev. Weddy James |
| Rev. Joseph .W. Mbilo | Rev. S.R. Mtema | Rev. Rainery .R. Haule |
| Rev. Ayubu .Y. Chaula | Rev. S. Sanga | Rev. Aloys Marwa |
| Rev. David .K. Mwaipopo | Rev. M. Mapunda | Rev. Amos .B. Ngonyani |
| Rev. Hamra .I. Kavenuke | Rev. D .P. Mtulo | Rev. S.H. Goliama |
| Rev. Julius .D. Kikoti | Rev. R.W. Mbangala | Rev. M.B. Kapinga |
| Rev. Hosea .Y. Kyando | Rev. E. Mwabulanga | Rev. Yolam Mwaluanda |

| Kanda Ya Mashariki Kusini | | |
|---|---|---|
| Rev. Dkt. Nicodemus Nyenye | Rev. C.Ngowi (Mdhamini) | |
| Rev. Dkt. A. Mwanjala | Rev. Simon Obedi | Rev. F.M. Makengwa |
| Rev. Anthony Aselga | Rev. Victoria Tungu | Rev. M.S Mgendanyi |
| Rev. Joel Kingu | Rev. M. Kisasa | Rev. S. Mpunga |
| Rev. John Kisoma | Rev. John Zacharia | Rev. D.G. Mwakila |
| Rev. Zakalia Chiza | Rev. Laban .E. Loje | Rev. A.M. Kwiyanda |
| Rev. Pascal B. Dede | Rev. Zaburi Joshua | Rev. F. Mwangela |
| Rev. Martin .J. Muumbe | Rev. Angell Mguluka | Rev. Pl .S. Mahiza |
| Rev. Ariel Mungereja | Rev. Mathew Munyagi | Rev. Isaya Chinyali |
| Rev. Hexaud .N. Ngimbudzi | Rev. Philemon Phiri | Rev. Aidan Mabuga |
| Rev. Sylivester Mhondo | Rev. J. Mwangomola | Rev. J.T. Mkinga |
| Rev. Isaya .M. Kaseleka | Rev. W.M. Mutaki | Rev. N. M. Mathayo |
| Rev. Chubwa .G. Vitus | Rev. John January | Rev. T. Mtumiah |
| Rev. Richard Lusinde | Rev. G. Mchaka | Rev. E.N. Swai |
| Rev. Samwel Mwankusye | Rev. G.W. Mraha | Rev. F.I. Mchezo |
| Rev. Jummanne Shabani | | |

| Kanda ya Kaskazini | | |
|---|---|---|
| Rev. Michael. D. Lyimo | Rev. Naftali Msoloka | Rev. E. Ngailo |
| Rev. Amos .M. Mbelwa | Rev. P.C. Kajuna | Rev. S. Shemzingwa |
| Rev. Elibariki .N. Moliel | Rev. Alfred Kalinga | Rev. Peter Shetuli |
| Rev. Shadrack Kingóri | Rev. Angela .R. Tarimo | Rev. W. Mkiramweni |
| Rev. Joseph Mlacha | Rev. E. Kabese | Rev. C. B. Lutabeka |
| Rev. Rogers Shemtambo | Specioza Joka Kuu | Rev. J.Chikianga |
| Rev. Emmanuel C. Ngairo | Rev S. M. Gissu | Rev. B. M. Rashid |

| Kurugenzi | | |
|---|---|---|
| Rev. Andindilile N Mwasice | Rev. C. Marialle | Rev. Sylivester Gissue |
| Ezekiel Kupasya | Rev.Dkt. M.Machibya | Rev. Gideon Malatila |

**MWISHO**

Imeandaliwa na Mwl. Dkt. Fulgence Binagwa kama Mshauri Mwelekezi
Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya Ofisi ya Katibu Mkuu-EAGT-Septemba 2019.